



Samia avunja rekodi Usalama wa Taifa



4

Idadi ya maofisa wakuu wa usalama waliobadilishwa ndani ya siku 1221.

Soma Uk. 6

Nape, Makamba 'OUT'



● Nnauye aponzwa na 'mdomo' wake, Makamba mhh!

Soma zaidi Uk. 12

Nape

Makamba

TRC kulipa milioni 4.8/- kila siku kusafisha mabehewa

soma Uk. 4



Soma Ndani

Muhimbili yarudisha matiti 'saa sita'

Soma Uk. 16

DC Dar atikiswa watoto kutekwa na kuuawa

MATUKIO ya kupotea, kutekwa na kuuawa kwa watoto katika Jiji la Dar es Salaam, yamemti-sha Mkuu wa Wilaya ya Teme-ke, na sasa achukua hatua.

Soma zaidi Uk. 8

Nape apata mtetezi, eti alilewa 'kahawa' Uk. 5

Tahariri/Katuni

Serikali iwajibike kufuatia Ripoti ya THBUB

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), moja ya vyombo mahsusi vilivyoundwa kusimamia na kulinda haki za binadamu, imetangaza ripoti yake na kueleza kuwa baadhi ya vituo vya Polisi nchini, vimegeuzwa kuwa kambi za mateso kwa watuhumiwa wakati wa mahojiano.

Matukio hayo ambayo sasa yanathibitishwa na THBUB, yamekuwa yakizungumzwa na wanchi na hata vyombo vya habari kuandika, lakini yakaonekana kama tetesi tu baada ya Jeshi la Polisi na mamlaka nyingine kukanusha.

THBUB kuyaeleza hayo hadharani, baada ya kufanya uchunguzi wake, kunalifanya Jeshi la Polisi na taasisi zingine za usalama zenye tabia hiyo kuacha mara moja.

Katika ripoti hiyo iliyokabidhiwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan, imeeleza mambo mengi yanayohusisha taasisi za serikali au viongozi wa serikali, kukiuka haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Mfano mmoja ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha aliyeelezwa kuwa aliamuru mtu kukamatwa

na kuwekwa ndani kinyume kabisa na taratibu zilizowekwa kisheria.

Inasikitisha kuona kuwa taasisi kama Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa zinaweza kufanya vitendio kama hivi.


Hakika mambo haya siyo matarajio ya dunia kuyasikia katika nchi inayojinasibu kuwa ni ya amani na inayofuata misingi ya utawala bora.

Pambazuko, kufuatia kuthibitika huko tunao-na kuwepo kwa sababu ya serikali kuchukua hatua kuonyesha kuwa kweli imedhamiria kulinda hadhi yake kwa kulinda na kutetea utawala bora.

Ripoti hii ya tume inaweka shaka kubwa kwa kauli za mara kwa mara za Jeshi la Polisi kuhusiana na masuala ya ulinzi wa watu na mali zao.

Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Polisi wanapaswa kuichukulia kwa uzito ripoti hii ya tume kwa sababu hizi si habari za mitaani – kama wanavyoziita wao, na kuzikanusha kila siku.

Tunachotarajia ni kuwa ripoti hii ya tume itafuatiwa na hatua za uwajibikaji wa wote ambao wametajwa kuhusika kwa kukiuka haki za binadamu na kuvunja misingi ya utawala bora.



Ofisi Kuu



*Mwonekano
wa jengo
zilipo Ofisi
za Gazeti la
Pambazuko
zilizopo
Mtaa wa
Mpakani
A, nyuma
ya Jengo
la Sayansi
Jijini Dar
es Salaam.
Gazeti hili
hutolewa
kila
Jumatatu.
(Picha na
Fidelis)
FELIX*

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435;
Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*



TRC kulipa milioni 4.8/- kila siku kusafisha mabehewa

Na Mwandishi WETU

ZAIDI ya shilingi milioni 144 zinatarajiwa kupipwa - kila mwezi - kwa kampuni iliyopewa kandarasi ya kufanya usafi kwenye mabehewa ya treni mpya ya SGR, baada ya kufunga mkataba na Kampuni ya Reli Tanzania (TRC).

Kiasi hicho ni sawa na shilingi 4.8 ambazo zitalipwa kila siku kwa kampuni hiyo ya usafi, Uchunguzi wa Pambazuko umebaini.

Mkataba huo ulisainiwa baina ya Kampuni ya Service Hub na TRC, siku chache kabla ya kuanza rasmi kwa safari za treni ya kisasa, inayotumia zaidi nishati ya umeme kuendeshwa (SGR).

Kiasi hicho cha zaidi ya shilingi milioni 144 kitalipwa kwa mwezi, endapo mabehewa yataongezeka hadi kufikia 28, baada ya kuanza kwa

safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Safari hiyo itaanza siku tatu zijazo – Julai 25.

Hivi sasa treni inayofanya kazi ya kusafisha abiria kati ya Dar es Salaam hadi Morogoro ina mabehewa 14.

Barua ya kuipa taarifa na kuitaka Service Hub kuanza kazi “mara moja,” baada ya makubaliano ya mkataba uliofungwa kati ya kampuni hizo mbili, na kusainiwa na Meneja Mkuu wa TRC, Gabriel Madenge, inaelekeza Kampuni ya Service Hub kuhakikisha inafanya kazi kwa uhakika na kwa weledi. Kampuni hiyo ilianza kazi rasmi Juni 14, 2024.

Tarehe hiyo ndiyo treni ya SGR ilianza safari zake rasmi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro.

Katika barua hiyo ambayo Pambazuko imeona, TRC inaipa taarifa Kampuni ya Service Hub yenye anwani yake Mtaa wa Ilala – Songea, Dar es Salaam, kuwa itakuwa ikilipwa malipo ya shilingi 172,083.33, kwa kuhudumia kila behewa kwa siku.

Gharama hizo zinajumuisha malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Kwamba kiasi hicho kitalipwa baada ya kuthibitika kuwa usafi wa mabehewa umefanyika kabla ya mabehewa hayo ya abiria kuanza safari na kila yanaporejea Dar es Salaam.

Hivi sasa treni hiyo, ikiwa na mabehewa 14, inafanya safari zake kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, hivyo kampuni ya usafi inatakiwa kuyasafisha yakiwa kituo kikuu cha Dar es Salaam na inapofika Morogoro kabla ya kupakia abiria kurudi.

Pambazuko linazo taarifa kuwa mwisho wa mwaka huu, TRC hueda itakuwa na mabehewa ya abiria 64 yanayofanya safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda mikoani.

Hata hivyo, haijaeleweka endapo Kampuni ya Service Hub itaendelea kusafisha mabehewa hayo yote, pamoja na kwamba barua yao ya kufunga mkataba inaonyesha kuwa watafanya kandarasi hiyo kwa miaka mitatu – kuanzia Juni 14, 2024 hadi Juni 13, 2027.



Wafanyakazi wa usafi katika Treni ya Kisasa ya Mwendokasi (SGR) wakiingia ndani ya behewa kufanya usafi baada ya kuwasili mkoani Morogoro hivi karibuni. (Picha na Fidelis FELIX)

Nape apata mtetezi, eti alilewa ‘kahawa’

Na Igo Al

MKEREKETWA “nambari wani” wa ile taasisi tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM), mmoja wa viongozi wastaafu wa serikali, Mzee Tai, jana aliwaita waandishi wa habari kuzungumzia mambo anuai ya chama chake.

Akiwa nyumbani kwake, Mtaa wa Mpakani A, Kijitonyama, Dar es Salaam, Mzee Tai kwanza aliwashukuru waandishi wa habari kwa kufika kwa wakati na kuwapongeza kwa kazi nzuri wanaoendelea kuzifanya kwa ujenzi wa taifa la Tanzania.

Mzee Tai, akiwa amevalia tisheti yake maarufu inayotambulisha ukereketwa wake kwa chama na “adabu,” pamoja na mapenzi yake kwa mwenyekiti wake, ambaye ni kiongozi wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwahimiza waandishi wa habari kuwa wazalendo na kuwaomba “kumsaidia mama (Samia)” ili afanye kazi zake bila kujawa msongo wa mawazo.

Alisema lengo kubwa la mkutano wake na waandishi wa habari ni kuwaeleza kwamba Nape Moses Nnauye, yule waziri mwenye dhamana ya habari, mawasiliano na teknolojia ya habari, ambaye hivi karibuni alitoa siri za chama chake hadharani – eti alikuwa amelewa.

Kwamba wanaomsakama Nape kwa kauli yake kuwa yeye amejaa mbinu za kupata ushindi kwenye uchaguzi wowote; iwe hata kwa njia haramu, hawamtendei haki, kwani aliyosema ndiyo njia zenyewe.

Mzee Tai akaendelea kusema kwamba njia hizo alizotaja Nape ndizo zinatumika kwa miaka nenda rudi, kuanzia Mtwara hadi Tanga, Lindi hadi Mwanza na kuwa kule Zanzibar, “ndiyo usiseme kabisa.”

Baada ya kueleza hayo, Mzee Tai

akaaga na kuwakaribisha chai na vitafunwa waandishi hao wa habari walioitikia wito wake.


Hata hivyo, kabla hajanyanyuka alipokuwa ameketi, mwandishi mmoja wa Pambazuko, akauliza; “Mzee Tai naomba utufahamishe na kuuambia umma wa Tanzania, “umesema Nape alikuwa amelewa, je, unajua alikuwa amekula ama kunywa nini kufikia hali hiyo?”

Mzee Tai akajibu; “alikuwa amekunywa kahawa, hivi nyie waandishi hamfanyi uchunguzi wenu kwa umakini, mnajua wakati anazungumza alikuwa wapi? Si alikuwa Kagera, kule anakotoka Tibaijuka, anakotoka Kaijage, anakotoka Byabato, anakotoka Muganyizi, kwani huko kuna kilevi gani – ni kahawa.”

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri inayoelezea na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa hapa na mhusika kutumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263.



Samia avunja rekodi Usalama wa Taifa



Rais Samia Suluhu Hassan

Na Waandishi WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan, leo akiwa ametimiza miezi 40 kamili madarakani, amevunja rekodi ya watangulizi wake wote; marais watano – kwa kufanya mabadiliko ya mara kwa mara ya wakuu wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS).

Mbali na kuvunja rekodi hiyo, pia waliowateuliwa na Rais Samia ndiyo wameweka rekodi nyingine ya kudumu kwa muda mfupi zaidi tangu kuanzishwa kwa idara hiyo nyeti kwa usalama wa watu, rasilimali na stawi wa Tanzania.

Anayeshikilia rekodi ya kuhudumu kwa muda mfupi zaidi ni Said Hussein Massoro ambaye amelitumikia taifa - kwa nafasi hiyo kwa muda wa miezi nane tu; kuanzia Januari hadi Agosti, 2023.

Mwingine anayemfuatia Massoro ni Balozi Ali Idi Siwa, ambaye alihudumu kwa miezi 11 pekee; huyu aliteuliwa na kuapishwa Agosti, 2023 na ku-

endelea na majukumu yake hadi mapema Julai, 2024.

Wote hawa wameteuliwa na kuondoka kwenye majukumu yao ndani ya uongozi wa Rais Samia, ambaye leo ametimiza siku 1,221 tangu alipoapa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Machi 19, 2021, kufuatia kifo cha mtangulizi wake, John Magufuli.

Rais Magufuli alifariki dunia Machi 17, 2021 kwa sababu zilizoelezwa na serikali kuwa ni shambulio la moyo.

Katika kipindi hicho cha uongozi wa Rais Samia, tayari Idara ya Usalama wa Taifa imekuwa na viongozi wanne; watatu wakiwa ni walioteuliwa na Rais Samia mwenyewe.

Je, mabadiliko hayo ya mara kwa mara ya wakuu wa idara hiyo yana afya kwa usalama na ustawi wa taifa na watu wake?

Hili ndilo swali – kutoka kwa wananchi, lililosukuma gazeti la Pambazuko kupata ufafanuzi wa wabobezi wa masuala ya kiusalama na ulinzi ambapo wanadai kuwa “mabadiliko hayo ni ya kawaida.”

Evarist Chahali ambaye ni Mtanzania anayeshi Scotland, mchambuzi wa masuala ya usalama, anasema kuwa zipo sababu mbili kubwa za kuwepo mabadiliko ya wakurugenzi wakuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Kwanza, ni mamlaka ya uteuzi ambayo ni Rais wa Jamhuri ya Muungano; ya pili, ni wateuliwa wenyewe.

Kwamba inaweza kuwa vigumu kwa rais aliyeipo madarakani kufanya kazi na mkurugenzi wa idara ambaye hajamteua yeye, hivyo kulazimika kuteua mwingine “atakiyeendana naye kikazi.”

Pia rais anaweza kufanya mabadiliko kutokana na mteuliwa kutenda kazi chini ya matarajio ya rais, hivyo kulazimika kumpumzisha ili kupata mwingine.

“Rais Samia alipoingia madarakani alimkuta Diwani Athumani ambaye alikuwa mteule wa Rais Magufuli, hivyo ilitarajiwa kuwa Rais Samia angemteua mtu mwingine kushika wadhifa huo kwa sababu katika utamaduni usio rasmi, wakuu wa nchi hupendelea kuwa na wakuu wa Idara za Usalama wa Taifa waliowateua wao wenyewe



Nape Nnauye alikaliwa kooni



Amos Makalla

Na Waandishi WETU

KAULI ya aliyekuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, inayoelezwa kubeba maana ya kuhalalisha haramu ya wizi wa kura, imemponza na sasa “katimuliwa.”

Wanaolaani kauli hiyo wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kuamua kumuwajibisha Nape, na kwamba hatua hiyo inatoa funzo kwa viongozi “wanaosigina” misingi ya demokrasia na Katiba ya Tanzania.

Maaskofu, wanazuoni, wanasiasa, waliozungumza na Pambazuko, wameeleza kufurahishwa kwao na uamuzi wa Rais Samia kutengua uwaziri wa Nape kwani unaonyesha namna anavyosimamia misingi ya utawala bora na demokrasia.

Akizungumzia uamuzi wa huo, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Padre Dkt. Charles Kitima, amesema kauli ya Nape ilileta shaka endapo uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa, utakaofanyika baadaye mwaka huu – 2024 na Uchaguzi Mkuu, 2025, utakuwa huru na wenye kubeba haki.

“Nilidhani tumejifunza kupitia Uchaguzi wa

Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ambao ulikuwa na uonevu mkubwa..”

“Hayo maneno ya Nape hayakuwa mazuri kwa sababu yanakumbusha watu yaliyotokea uchaguzi wa 2019 na 2020, na yanakwenda kinyume na kauli ya Rais Samia ambaye amekuwa akiisitiza uchaguzi ujao utakuwa huru na wa haki,” amesema Dkt. Kitima.

Askofu Mkuu (mstaafu) wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dkt. Fredrick Shoo ameeleza kufurahishwa na uamuzi wa Rais Samia akieleza kwamba alisikitishwa na kauli ya Nape na kwamba ilionyesha hofu endapo uchaguzi ujao; wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, utakuwa huru na wa haki.

“Ilinisikitisha na kunishtua sana. Hii ina maana anatuambia Watanzania tutarajie yaleyale machafu yaliyofanyika 2019 na 2020...”

“Kauli ya Nape ilifuta kabisa hata msimamo wa mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na ahadi yake kuwa chaguzi zijazo zitakuwa huru na za haki...”

“Pamoja na jitihada za Katibu wa Halmashauri Kuu, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, kujaribu kukanusha haya, tuisahau kuwa aliyetamka maneno haya alikuwa ni Waziri wa Serikali ya CCM,” amesema Dkt. Shoo.

Askofu huyo akaendelea; “sisi tumeshasema hatutaki kuona uchafuzi kama ule uliopita ukijirudia, lakini kumbe kunaweza kutokea yaleyale kwa kuwepo watu kama Nape ambao wanafikiri Watanzania wote ni wajinga na wanaweza kuwafanyia watakavyo.”

Maaskofu hao wamekuwa na msimamo mmoja wakisema kwamba waliamini baada ya kauli ya Nape kusambaa na yeye kuona amepotoka, angechukua uamuzi wa kuwajibika, badala ya kushubiri ngazi za uteuzi kufanya hivyo.

Chadema wanena

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mnyika, aliliambia



Habari

DC Temeke atikiswa utekaji, mauaji watoto



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda

Na Hellen NGOROMERA

MATUKIO ya kupotea, kutekwa na kuuawa kwa watoto katika Jiji la Dar es Salaam, yamemtisha Mkuu wa Wilaya ya Temeke, na sasa achukua hatua.

Mkuu huyo wa wilaya, Sixtus Mapunda, pamoja na kutikiswa zaidi na matukio hayo ndani ya eneo lake la utendaji, amesikitishwa na wahalafu hao kutumia “chips-mayai” kurubuni watoto, kuwateka, kuwalawiti na hata kuwaua.

Akizungumza na Pambazuko, Mapunda amethibitisha kuwa hadi wiki iliyopita watoto watatu walikuwa wameripotiwa kutekwa na kisha kuawa.

Mkuu huyo wa wilaya akifafanua zaidi amesema kuwa Machi 13, mwaka huu - kati ya saa nane na saa tisa alasiri, watoto wawili wa kike, walikutwa wakicheza eneo la Mbagala Kuu na mtekaji aliwachukua akiwaambia anakwenda kuwanunulia “chips – kuku” na nguo, nao walimfuata.

Mapunda amesema mtekaji aliongozana

na watoto hao kwa mguu na walipofika eneo la Zakhem, mmoja wao alisema amechoka ndipo alimwacha na kuongozana na aliyebacki.

Mapunda amesema mtoto aliyeachwa, alio kotwa na wasamaria wema huku mwili wa mwenzake ukiokotwa kesho yake eneo la Mbagala, ukiwa umetelekezwa kichakani.

Uchunguzi ulionyesha kuwa mtoto huyo alikuwa umeingiliwa.

Ameongeza kuwa tukio jingine lilitokea Aprili 8, mwaka huu eneo la Mbagala, Zakhem baada ya mtoto wa kike wa miaka tisa kupoteana na ndugu zake na baadaye saa 3.30 usiku kukutwa akiwa hai, lakini uchunguzi ulibaini kuwa alikuwa ameingiliwa.

“Katika tukio hili, mtoto huyo alisalimika, na tunahisi mfanyaji wa vitendo hivyo huwaziba pumzi na kwa kuwa mtoto ana umri wa kujitambua huenda alikuwa akipambana ndipo alifanikiwa kunasuka,” amesema mkuu huyo wa wilaya.

Amesema mtoto huyo anaendelea kutoa ushirikiano kuwezesha kuwatambua na kuwakamata watuhumiwa.

Tukio jingine ambalo lilisababisha kifo lime tokea Julai 8, mwaka huu huko Mbagala baada ya mtoto mmoja kuingiliwa kimwili kisha kuuawa.

Mapunda amesema mtoto huyo wa kike ambaye alifikwa na mauti, alikwenda Mbagala kumtembelea mjomba wake akitokea Wilaya ya Rufiji, Pwani.

Mkuu huyo wa wilaya ameeleza kutokana na hali hiyo, ofisi yake imechukua hatua ya kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu katika shule ili kuwafanya watoto kuwa na uelewa wa mambo hayo na kujilinda.

“Tumeona kwamba kinachokosekana hapa ni elimu, hivyo tumeanza kutoa elimu kushirikiana na watendaji wa mitaa, viongozi wa dini na kadhalika. Tuna imani huyu mtu atakamatwa muda si mrefu,” amesema Mapunda.

Amesema mtu huyo anayefanya uhalifu huo anaonekana kufahamu maeneo mengi na kwamba matukio yake huyafanya mchana.

Kutokana na matukio hayo, baadhi ya wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wamekosa amani na kufanya wengine kuzuia watoto wao kwenda shule na wachache kuwawekea ulinzi kila wanapokwenda.

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Ikulu ya Marekani

Taswira ya hekaheka za uchaguzi Marekani

KUNA sintofahamu kubwa – kuhusu masuala ya uchaguzi mkuu, inayoendelea nchini Marekani.

Kwa upande mmoja, jaribio la mauaji dhidi ya Rais wa zamani wa nchi hiyo, Donald Trump linaendelea kuumiza vichwa na kuacha maswali mengi kuliko majibu.

Trump ambaye pia ni mgombea wa urais wa Marekani kwa tiketi ya chama cha kihafidhina cha Republican, alikumbwa na masahibu ya kushambuliwa kwa risasi Julai 13, mwaka, aliporushiwa risasi wakati akihutubia mkutano wa kampeni.

Kwamba shambulio hilo lilitokea licha ya ulinzi mkali alionao Trump, siyo tu kama rais wa zamani, bali pia mgombea urais, imezua maswali mengi ya siyo na majibu.

Lakini, tukio hilo pia limetokea wakati Marekani ikiwa katika hekaheka za uchaguzi mkuu utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Sambamba na hilo, jaribio hilo la mauaji dhidi ya Trump limetokea wakati taifa hilo likiwa limegawanyika mno kiitikadi.

Upinzani baina ya Republican ya Trump na chama tawala cha Democrats cha Rais Joe Biden, umevuka mipaka na kuchukua taswira ya uhasama baina ya vyama hivyo na wafuasi wake.

Ndio maana mara baada ya tukio hilo, viongozi kadhaa wa Republican na wafuasi wao, walianza kudai kuwa jaribio hilo la mauaji dhidi ya Trump lilikuwa na mkono wa Rais Biden.

Lakini pengine kibaya zaidi ni ukweli kwamba jaribio hilo limetokea katika zama hatari za kusambaa kwa habari za uongo na kutunga, ambapo husambaa kwa kasi kuliko ukweli.

Mitandao ya kijamii inawezesha mtu yeyote yule kuwa mwanahabari, fursa ambayo baadhi ya watumiaji wa mitandao hiyo wanaitumia kwa manufaa, lakini pia kuna idadi kubwa tu wanaoitumia vibaya.

Kwa mfano, mara baada ya aliyefanya shambulio hilo kufahamika na picha yake kuwekwa mtandaoni, mtu mmoja alirekodi video yenye ujumbe kwamba ametumwa na Rais Biden kumuua Trump.


Video hiyo ilisambaa kwa kasi na kuwafikia mamilioni ya watu kabla ya kuwekwa taarifa kuwa ni habari ya uongo. Ipuuzwe.

Kwa upande mwingine, tayari sintofahamu miongoni mwa Democrats sasa imemalizwa baada ya Rais Joe Biden kutangaza jana kwamba hatasimama kugombea nafasi hiyo ya kuongoza Marekani.

Awali, kulionekana kuwepo baadhi ya viongozi wa chama hicho wakimshauri Rais Biden ajiondoe kwenye kinyang'anyiro cha kuwania urais kutokana na kufanya vibaya kwenye mdahalo kati yake na Trump, na mwenendo usioridhisha wa kura za maoni.

Wiki zijazo zinatarajiwa kuwa na hekaheka nyingi kuhusiana na tukio hilo kwa Trump pamoja na uchaguzi mkuu kwa ujumla.

https://instagram.com/evarist_chahali



Tafakuri ya Bagonza

Biden, Trump – wote minne tena! Wape kura siyo risasi

Na Dkt. Benson BAGONZA

JUMAMOSI iliyopita – Julai 13, 2024, dunia ilitaharuki kusikia huko Marekani, mgombea urais wa chama cha Republican, Donald Trump amepigwa risasi jukwaani wakati wa mkutano.

Wagombea wakubwa wawili katika uchaguzi wa Marekani; Joe Biden, rais wa sasa na Donald Trump wanaomba kuongoza kwa miaka mingine minne.

Trump ni kama alisahau kitu White House na Biden ni kama kuna kitu hajafanya, anatamani apate muda zaidi ili akifanye.

Nayatafakari haya kwenye mchuano huo wa kupambana kuongoza Marekani;

Kwamba risasi aliyopigwa Donald Trump ni “kura ya risasi” kuliko kuwa “risasi ya kura”. Wapo watakaompa kura kwa sababu ya kupigwa risasi. Tujiepushe na zimwi la risasi kwa wapinzani wetu. Risasi hugeuka kuwa kura.

Kwamba kifungo na risasi ni viwanda vya kura katika chaguzi. Hata mgombea bomu akipigwa risasi wakati wa kampeni au kuwekwa mahabusu, kura zake huongezeka.

Kwamba wapo wanaodhani kuwa huenda Trump alipanga apigwe risasi ili kuongeza kura

zake.

Kwamba Trump na Biden wote ni wazee. Biden anasahau njia ya kupanda ngazi kuingia kwenye ndege wakati Trump anasahau anagombea kuwa nani kwa sababu bado anajiona ni rais!

Kwamba wagombea wote wawili wanadhihirisha kitu kimoja muhimu; Marekani inaongozwa na taasisi kuliko watu. Hata chizi anaweza kuwa Rais wa Marekani kwa sababu siyo yeye anayeongoza.

Kwamba uhuru usio na mipaka unastawisha utumwa wa taasisi; yaani taasisi inamtumikia mtu, siyo mtu kutumikia taasisi. Uhuru kama wetu wenye mipaka unakuza utumwa mstaarabu. Tunahitaji kuazimana, lakini tukumbuke kurudisha.

Kwamba risasi ni silaha ya mkandamizaji. Mkandamizwaji hutumia meno na ulimi. Anayekuuzia risasi leo, kesho anamuuzia adui yako fulana ya kuzuia risasi aliyokuuzia jana. Tunahitaji vita ya maneno siyo risasi. Hakuna fulana ya kuzuia maneno.

Kwamba kKutumia risasi kumnyamazisha Trump ni kumpendelea. Trump ni zao la “ndoto ya Amerika” inayoamini katika kutumia risasi kuzima ndoto nyingine. Ndoto ya Amerika inazimwa na ndoto ya Amerika.

Kwamba Trump siyo tatizo. Wanaomfuata ndio tatizo. Hakuna kazi nzito kama kumbadili muumini aliyemwamini nabii au mtume feki. Atacha wali nyumbani aende kula kinyesi kwa nabii wake na awacheke wanaomshangaa. Kampeini za Amerika hazina “unatuachaje,” bali “Amerika kwanza” na Mungu baadaye.

Kimsingi, vyama vya Republican na Democrat vimekosa wagombea. Trump na Biden ni makuadi na madalali wa kuuza gulioni ndoto ya Amerika kwa nchi zisizo na ndoto zake.

Gulio humnufaisha muuzaji kuliko mnunuzi. Wote wawili wanakubaliana kuwa na Amerika kwanza na iliyo imara hata kama wao siyo imara kiakili na kimwili.

(safu hii iliandikwa kabla ya Rais Biden hajajiondoa kwenye kinyang'anyiro jana)

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Donald Trump

Rais Joe Biden



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Utitiri michango shule za serikali mzigo kwa mzazi

njia mbadala ya 'kuwakamua' wazazi kwa njia za michango ambayo haina sura ya hiyari, bali ni lazima.

Katika Shule ya Sekondari Umbwe iliyoko Moshi, Kilimanjaro, mzazi mmoja alilazimika kulipa shilingi 50,000 kwa ajili ya ujenzi wa ukuta, shilingi 10,000 kwa ajili ya jenereta, na shilingi 30,000 kwa ajili ya tuition kwa nusu muhula.

Kama hiyo haitoshi, mzazi huyo alielezwa kuchangia ununuzi wa king'amuzi shilingi 3,000 jumla ni shilingi 93,000 kwa michango yote, na endapo italipwa kwa mihula miwili, basi atalazimika kukamiliwa shilingi 186,000.

Katika mazingira yoyote, kiasi hiki ni kikubwa na kuwa mzigo kwa wazazi na walezi, licha ya serikali kutangaza kuondoa ada.

Swali linabaki, je, nia ya serikali ya kuondoa ada imefanikiwa? Inavyoonekana michango imekuwa aina Fulani ya ada, hivyo kuendelea kufanya maisha ya familia zinazosomesha kuwa magumu.

Huu ubunifu wa shule kupata njia nyingine za kukusanya fedha, haukubaliki. Lazima ukemewe.

Malalamiko haya ya wazazi hayako kwenye shule moja pekee, bali yanasikika sehemu nyingi na kutokana na sababu hiyo, ni vyema kukawepo uwazi na uwajibikaji ili kuhakikisha michango hiyo inasimamiwa vizuri na haigeuki kuwa mzigo kwa wazazi.

Vilevile, serikali inapaswa kutafuta njia za kuongeza bajeti ya elimu ili shule zisiwe na ulazima wa kutegemea michango ya wazazi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kila siku.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Waziri wa Elimu Prof. Adolf Mkenda

NAPONGEZA mpango wa Tanzania kuondoa ada kwa shule za umma kuanzia shule za awali hadi kidato cha sita.


Lengo kuu la hatua hii lilikuwa ni kupunguza mzigo kwa wananchi na kuhakikisha kila mtooto ana fursa ya kupata elimu, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Hii ni kwa sababu elimu ndio mtaji muhimu kwa watu, hususan kwa wale wanaotoka familia masikini. Mtu mwenye elimu, mara nyingi anakuwa tofauti sana na viumbe wengine.

Hata hivyo, licha ya nia njema ya serikali, imebainika kuwa michango iliyobaki kwenye shule hizo imegeuka kuwa mzigo mkubwa kwa wazazi na walezi, kiasi cha kufanya hatua ya kuondoa ada ionekane haina tija.

Michango hii ni pamoja na gharama za ujenzi wa miundombinu kama kuta za shule, kununua jenereta, na ada za ziada za masomo (tuition) ambazo kwa pamoja zinaweza kufikia au hata kuzidi kiasi kilichokuwa kinatozwa kama ada hapa awali.

Ipo mifano mingi ya shule za sekondari za juu hapa nchini ambazo wakuu wake wamebuni



Nape Nnauye, January Makamba 'OUT'

Na Mwandishi WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko makubwa ya baraza lake la mawaziri, huku akitengua dhamana za mawaziri wawili waandamizi; Nape Moses Nnauye na January Yusuf Makamba.

Mawaziri hao wawili waandamizi, ndiyo walioondolewa kwenye nafasi walizokuwa wakizishikilia hadi jana usiku, Jumapili; Julai 21, 2024 - dakika 39 kabla ya tarehe kupinduka – na kuanza siku nyingine, Jumatatu - Julai 22, 2024.

Nape alikuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, wakati Makamba alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mawaziri hao wawili, taarifa kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu imeeleza kuwa uteuzi wao umetenguliwa.

Sababu Nape kutenguliwa

Pamoja na kwamba taarifa ya Ikulu, kama ilivyo kawaida, haikueleza sababu za kutenguliwa kwa mawaziri hao, lakini angalau Watanzania wanatambua kuwa Nape ameponzwa na mdomo wake.

Kwamba Nape hivi karibuni aliweka serikali na chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika wakati mgumu kufuatia kauli yake inayoendelea kutafsiriwa kuwa ushindi wa chama hicho tawala, hutokana na “wizi wa kura.”

Kufuatia kauli hiyo aliyoitoa eneo la Kashai, Bukoba, hivi karibuni, Nape alisema yeye ni bingwa wa kusaka ushindi katika uchaguzi na kwamba kura zinazopigwa sandukuni siyo lazima zimfanye mgombea kushinda, bali anayehesabu na anayetangaza matokeo.

Pambazuko limeelezwa kuwa kauli hiyo ya Nape ilimkera Rais Samia na kwamba mitazamo ya wana-nchi, wanazuoni, viongozi wa dini, wanaharakati na wanasiasa, kulaani kauli ile, imechochea zaidi kuchukua hatua ya kumtengua.

Je, Makamba amekwama wapi?

Kuhusu Makamba, muda mfupi wakati Pambazuko linajiandaa kwenda mitamboni, lilidokezwa kuwa utenguzi wa waziri huyo wa mambo ya nje, haikuwa hatua ambayo inatarajiwa.

“Nikwambie tu kwamba kutenguliwa kwa Makamba hakukutarajiwa, kwani huyu Makamba alikuwa mtu wa karibu sana na Mama (Rais Samia), sasa sijui ni kitu gani kimetokea...”

“Hata hivyo, hizi nafasi zina mambo mengi sana, lakini pia huenda ni majungu na figisu za wenzake ambao wanamuona ni mwiba na kikwazo kwa nafasi ya urais kwao, baada ya Rais Samia,” amesema ofisa mmoja mwandamizi ndani ya Ikulu.

Amesema kuwa Makamba, katika kipindi cha uwaziri wa mambo ya nje, alijenga kuaminika na kuonekana msaidizi mkubwa wa shughuli za rais, hasa kwenye ushirikiano na mataifa mengine, lakini sasa “yametokea ya kutokea, yasiyotarajiwa.”

Huku akisisitiza kutotajwa jina gazetini, amesema kutenguliwa kwa Makamba kutaleta mshangao mkubwa kwa wengi, na hata maba lozi, ambao walikuwa wakimwamini zaidi kuliko mawaziri wengine wengi kabla yake.

Mkeka wa mabadiliko ya mawaziri, viongozi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi, utenguzi na uhamisho wa viongozi mbalimbali kama inavyosomeka hapa;

Jerry William Silaa, ameteuliwa kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kabla ya uteuzi huu Mhe. Silaa alikuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, anachukua nafasi ya Nape Moses Nnauye, ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Deogratius John Ndejemi, ameteuliwa kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kabla ya uteuzi huu Mhe. Ndejemi alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

Ridhiwani Jakaya Kikwete, ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu). Kabla ya uteuzi huu Kikwete alikuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Balozi Mahmoud Thabit Kombo, ameteuliwa kuwa Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kabla ya uteuzi huu Balozi Kombo alikuwa Balozi wa Tanzania nchini Italia, anachukua nafasi ya January Yusuf Makamba, ambaye uteuzi wake umetenguliwa;

Cosato David Chumi, ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Chumi anachukua nafasi ya Balozi

Inaendelea Uk. 20

Kona ya Dkt. Bisimba

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

TANGU wiki iliyopita nilianza kutafakari suala la chaguzi zilizopo mbele yetu; yaani Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu, 2024 na Uchaguzi Mkuu mwaka ujao, 2025.

Nilijiuliza wapiga kura tunajiandaa je ili tuwe tayari kwa kujiandikisha na kupata taarifa zote muhimu.

Wakati nikiwa katika tafakari hiyo, nikakuta na video kwenye mitandao ya kijamii ikimonyesha Nape Nnauye akiwa anazungumza na raia huko mkoani Kagera.

Katika video hiyo, alikuwa akijieleza bila wasiwasi kabisa kuwa mbunge wa sehemu aliyekuwepo asiwe na hofu kwani atarudi tu kwenye kiti hicho kwani yeye (Nape) ni mtaalamu wa mambo ya uchaguzi na kwamba zipo mbinu zinazotumika ambazo alisema zipo za halali na nusu halali na haramu, ili kushinda.

Alijieleza pia kuwa ushindi hautokani tu na kura za ndani ya boksi ambazo zimepigwa, bali inategemea na anayehesabu na kutangaza matokeo.

Niliposikia hayo sikuamini kuwa mtu wa haiba yake na wadhifa wake, anaweza kusema maneno yale tena hadharani.

Niliona ni dharau na kejeli ya kupitiliza kwa sisi wapiga kura.

Alionyesha kuwa kumbe hakuna sababu ya kujiandaa kupiga kura kwani matokeo huweza kutengenezwa tu.

Nilijiuliza dharau kama hii inatokana na nini hasa. Nikakumbuka kauli yake ya huyuhuyu Nape mwaka 2015, aliposema watatumia hata 'goli la mkono' kushinda uchaguzi. Nikakumbuka yale yaliyojitokeza mwaka 2019 na 2020 ambapo uchaguzi ule ulichafuliwa.

Nimesimkia Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, akisema kauli ya Nape siyo msimamo wa chama chao.

Nilichojiuliza iwapo huo siyo msimamo wa chama, huyu mwanachama wao alipata wapi mamlaka ya kuongea tena kwa jeuri kubwa kiasi kile na bila kuchukuliwa hatua yoyote?

Iwapo kauli hiyo siyo ya chama, nadhani hai-toshi tu chama kuikataa bila kumwajibisha aliyetoa kauli hiyo.

Kwa uzito wa kauli ile, fedheha na taharuki

Nape hakustahili kuendelea kuongoza

iliyozua isingetosha kuikanusha hiyo kauli bila hata hatua madhubuti kuchukuliwa.

Nape mwenyewe amejitokeza na kujionyesha kuomba msamaha. Nilipomsikiliza niliona bora angekaa kimya kwani kwangu mimi alikuwa anahalalisha kile alichokisema.

Anakubali kuwa alisema vile kwa kudhamiria kuwa ni utani. Lakini najiuliza, mtani wake ni nani katika masuala mazito ya kidemokrasia nchini?

Kuna mtu mmoja nimemsikia akisema labda tumpungeze Nape kwa kuwa mkweli kwani aliyoyasema yalitoka moyoni na ndivyo ilivyo.

Sasa yaliyotarajiwa na Watanzania, ndiyo yamefanywa na mamlaka iliyomteua kumchukulia hatua kwa kutengua uteuzi, na ndicho wananchi walikuwa wakisubiri kwa hamu.

Nape sasa amewajibishwa, ingawa bado sisi wapiga kura tuna hasira naye.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatika-na kwa namba 0713 337240.



Nape Nnauye



Samia avunja rekodi Usalama wa Taifa

Inatoka Uk. 6

badala ya kurithi, isipokuwa pale katiba inapokatiza,” amesema Chahali.

Chahali anasema kwamba katika Tanzania, hata kama mabadiliko yatafanywa wakati nchi inapokaribia uchaguzi, hakuna maana kwamba idara hiyo inasukumwa kusaidia chama tawala.

“Kuteuliwa kwa mkuu wa usalama wa taifa wa sasa (Selemani Mombo), kusionekane kuwa ni maandalizi ya kufanya figisu wakati wa uchaguzi ili Chama Cha Mapinduzi (CCM) kishinde kwa urahisi, la hashu, nadhani tu amepewa ili kuhakikisha utatuzi wa changamoto wakati wa uchaguzi, kwa kuwa rais kaona mazingira yajayo yanahitaji mtu wa aina yake,” ameingiza Chahali.

Mtaalamu na mchambuzi wa mambo ya utawala na uongozi, Dkt. Albanie Marcos amelieleza Pambazuko kuwa mabadiliko ya wakuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, huenda yanafanywa mara kwa mara kwa sababu kubwa tatu; kwanza kupata mtu sahihi, mtu mwenye weledi na zaidi sana mzalendo wa hali ya juu.

“Rais Samia anafanya hivyo kwa kuwa anataka apate mtu wa kwenda na matarajio yake, akiona mtu anamchelewesha, basi ana uhuru na katiba inamruhusu, kufanya mabadiliko, bila kujali ni muda gani kiongozi aliyepo amehudumu,” amesema Dkt. Marcos.

Miongoni mwa majukumu makubwa ya idara hii – kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania, yanahusu zaidi kutafiti kwa usahihi, kufuatilia, kusimamia na kushauri vyema kuhusu ulinzi wa rasilimali za taifa, kuzuia kuvuja kwa taarifa za siri za ndani ya nchi na kulinda uhai wa watu.

Dkt. Marcos pia ameeleza kuwa mabadiliko ya viongozi wa idara hiyo hufanywa na rais kwa kuzingatia hali halisi ya siasa za nyakati, usalama wa nchi na haki za binadamu.

Mtaalamu na mchambuzi wa siasa na utawala kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. George Kahangwa amelieleza Pambazuko kuwa mabadiliko hufanyika katika idara hiyo kwa kutegemea mazingira na uwezo wa kiongozi kukabili matukio ya wakati.

Anasema kutokana na unyeti wa Idara ya Us-



Ikulu Chamwino, Dodoma

alama wa Taifa, kila rais anayeingia madarakani anakuwa na matamanio yake na kupenda kufanya kazi na mtu anayemuelewa na kumwamini zaidi, hivyo mabadiliko ni lazima.

“Pia mabadiliko haya yanaweza kufanyika kwa sababu tu wahusika hawawajibiki ipasavyo kukidhi mahitaji ya nyakati na taarifa zinazopeleka kwa kwa rais ndizo zinazomuelekeza kama huyu anahitaji kuendelea naye au la, ni kama kocha anavyopanga timu yake, ana uwezo wa kutumia mchezaji amtakaye yeye wakati wowote...”

“Usalama wa Taifa unahusu uhai wa watu, unahusu Uchumi - na tunaona kasi inayoelekezwa kwenye kuvutia wawekezaji, inahusu siasa na tunaona namna wanavyoelekeza kutimiza nia ya Rais Samia, sasa akibaini mtu anayemtegemea hampi taarifa sahihi za kumsaidia na ana mwelekeo wa kujali kundi fulani la kisiasa, hawezi kuendela kumvumilia,” anasema mwanazuoni huyo.

Anasema pamoja na kwamba Rais Samia peke ndiye anajua kinachomsukuma kufanya mabadiliko ya wakuu wa idara hiyo, suala jingine linalosababisha mabadiliko katika idara hiyo nyeti ni mwelekeo wa uchaguzi ambapo nafasi hii inahusika moja kwa moja na udhibiti wa matukio

Inaendelea Uk. 20

Nape Nnauye alikaliwa kooni



Shangwe Ayo

Inatoka Uk. 7

Pambazuko mapema kwamba alichokisema Nape kinaonyesha ndiyo msimamo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), licha ya utaratibu huo kutokuwa hadharani, hadi alipouweka wazi Nape.

Mnyika jana alisema umma utakuwa umepokea kwa furaha uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kutengua uteuzi wa waziri huyo na kutaka chama chake nacho kimchukulie hatua kwa kuwa kauli hiyo “haikutakiwa kutolewa hadharani.” “Pamoja na hayo, umma ujiandae kudai haki kwani kuna kila dalili kwamba akina Nape wanataka kuturudisha nyuma kama tulivyoshuhudia uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020,” ameongeza Mnyika.

ACT-Wazalendo

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma wa ACT- Wazalendo, Shangwe Ayo, ameliambia Pambazuko kuwa kauli ya Nape hai-kuwa ya bahati mbaya, ilidhamiriwa na kwamba kutenguliwa kwake kulitarajiwa.

Shangwe kauli ya Nape ilikuwa inadhihirisha msimamo wa Nape na chama chake, ndiyo huo wa kupata ushindi kwa njia yoyote, hata ikiwamo haramu – ya wizi wa kura.

Amesema ACT-Wazalendo kinakemea vika-li kauli ya Nape na kwamba chama chake kinge-shangaa ikiwa Nape asingeadhibiwa kwa kuondolewa nafasi ya uwaziri.

LHRC walaani

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dkt. Anna Henga, awali akizungumza na Pambazuko alilaani kauli hiyo na kusema ina kila dalili za kuwagawa wananchi, na kubeba maana ya kuvuruga uchaguzi ujao.

“Alichokisema Nape ni dharau kubwa kwa Watanzania na kwa demokrasia, ni kauli mbaya inayovunja mioyo ya wananchi kuamini thamani ya sanduku la kura, hata kama tayari chama chake kimemkana,” ameongeza msomi huyo wa sheria.

Mtazamo wa Mutungi

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, akizungumza na Pambazuko mapema juzi alisema ni vyema vyombo vya habari vikaacha kuripoti kuhusu kauli ya Nape kwa kuwa “haisaidii Tanzania.”

“Jambo hili ni vyema vyombo vya habari mliache, kuendelea kuliandika ni kulikuza kwa sababu haliisaidii nchi, dawa yake ni kulikalia kimya tu, msiandike” alisema Jaji Mutungi.

Msimamo wa Makalla, CCM

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Amos Makalla, amekitenga chama chake na kauli ya Nape na kusema ushindi wa chama chake “kamwe hautegeei mbeleko” kushinda uchaguzi.

“Mara zote CCM hujipanga kushinda kwa haki. Narudia tena, CCM aihitaji mbeleko, sisi tutashinda kwa haki kwa sababu tunayo rekodi nzuri ya kuwaletea wananchi maendeleo,” amesisitiza Makalla.

Kauli ya Nape

Hivi karibuni, Nape Nnauye akizungumza na wananchi katika Kata ya Kashai, Bukoba Mjini, alisema kuwa mshindi katika uchaguzi siyo lazima utokane na kura zilizopigwa, bali hutegemea anayehesabu na anayetangaza matokeo.

“Kuna mbinu nyingi katika uchaguzi, kuna mbinu halali, kuna nusu halali na kuna mbinu haramu na zote zinaweza kutumika ili mradi tu ukishamaliza kuzitumia, unamwambia Mwenyezi Mungu nisamehe tu...”

“Kwa hiyo, wanaotaka kushindana naye (Mbunge wa Bukoba Mjini, Stephen Byabato), wajipange, mmenielewa eeh, wajipange na Mwenyezi Mungu atatusaidia.”

Muhimbili yarudisha matiti ‘saa sita’



Daktari bingwa wa upasuaji rekebishi na urembo wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Upanga (Plastic and Cosmetic Surgeon), Edwin Mrema, akionyesha picha zilizofanyiwa upasuaji rekebishi na urembo kabla na baada ya upasuaji katika Banda lao lililopo kwenye Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) katika Viwanja vya Julius Nyerere mwishoni mwa wiki. (Picha na Fidelis FELIX)

Na Arodia PETER

WATAALAM wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Upanga, Dar es Salaam wamefanikiwa kuwafanyia upasuaji wanawake wenye matiti makubwa yaliyoanguka na kuyaweka kwenye ‘saizi’ ndogo maarufu ‘saa sita’.

Upasuaji huo hufanywa kupitia kitengo cha upasuaji rekebishi, urembo na majeraha ya moto kupitia huduma za kibingwa na kibobezi hospitalini hapo.

Huduma hiyo inayoonekana kuwavutia watu wengi kwani katika kipindi cha miaka minne iliyopita takibani watu 200 wamejitokeza kufanyiwa upasuaji rekebishi katika hospitali hiyo.

Akizungumza na Pambazuko wiki iliyopita, daktari bingwa wa upasuaji rekebishi na urembo wa hospitali hiyo, Dkt. Edwin Mrema, alisema huduma hizo ni kwa ajili ya kuboresha ma-

umbile ya mwili.

Moja ya huduma zinazotolewa kupitia upasuaji huo ni kupunguza au kuongeza ukubwa wa matiti na kuyaweka kwenye umbile la kuvutia kulingana na matakwa ya mteja.

Mbali na matiti, alisema wanafanya upasuaji wa urembo wa kuondoa kitambi na kutengeneza maumbile kwa wanawake na wanaume.

Alisema kitengo hicho cha upasuaji wa urembo kimekuwepo Muhimbili kwa zaidi ya miaka 20, lakini kutokana na watu wengi nchini kuto kuwa na taarifa za kutosha, wamekuwa waki fuata huduma hizo nje ya nchi katika mataifa ya India, Marekani na nchi nyingine za Ulaya.

“Kama matiti ni madogo tunayaweka kwenye ukubwa na makubwa yanakuwa madogo. Nichukue nafasi hii kuwaambia Watanzania kwamba serikali imesomesha wataalam wengi na wapo kwa ajili ya kutoa huduma...”

“Huduma nyingi ambazo zamani zilipatikana nje ya nchi kama India na Marekani, kwa sasa zinapatikana hapa nchini katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, kwa hiyo badala ya kupeleka fedha nje ya nchi, watu waje kupata huduma hapa,” alisema Dkt. Mrema.

Daktari huyo alibainisha kuwa huduma za kurekebisha maumbile hazina madhara, isipokuwa ni kitu kigeni, ndiyo maana watu wanakuwa na wasiwasi.

“Kitu kikiwa kipya, watu wanakuwa na wasiwasi nacho, ndiyo maana tupo kutoa elimu kwa jamii ili watu waelewe kwamba siyo tu matibabu ya watu wanaoungua moto, kupata vidonda kwa ajali za barabarani, makovu ya kila aina, lakini pia tunatoa tiba ya urembo vilevile kwa mtu anayetaka muonekano wake ubadilike,” aliongeza.

Aidha, huduma za upasuaji rekebishi zinahusisha majeraha yatokanayo na ajali, uzazi, moto, saratani na maabukizi ili kurudisha viungo kwenye hali yake.

Pia huduma hizo zinahusisha matatizo ya mdomo sungura, hitilafu za mikono na vidole, saratani ya matiti, makovu, vipara vitokanavyo na majeraha na upasuaji mwingine wa kitabibu.

Tishio saratani ya shingo ya kizazi lapungua

Na Hellen NGOROMERA

HOFU ya Tanzania kuwa na idadi kubwa ya wasichana wenye magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi, imepungua, Pambazuko limeelezwa.

Kampeni iliyoanzishwa na serikali, imeweze sha hofu hiyo kupungua baada ya kuwepo mafanikio – na kuvuka malengo, ya kuchanja wasichana wengi, hasa wanafunzi.

Ofisa Programu Mpango wa Taifa wa Chanjo, Lotalis Gadau (pichani), ameliambia gazeti hili kuwa kampeni hiyo imevuka lengo kwa kuchanja asilimia 96 ya wasichana wenye umri kati ya miaka tisa hadi 14 nchi nzima.

“Wakati tunaanza kutoa chanjo hii, tulilenga kuwachanja watoto milioni 4.9 sawa na asilimia 80 ya watoto wenye umri huo nchini, lakini kutokana na hamasa kubwa, tumefanikiwa kuvuka lengo kwa kuwafikia wengi kabla ya kipindi tulichojiipangia kukamilisha kampeni ambacho ni Desemba mwaka huu,” amesema Lotalis.

Chanjo hiyo ilianza kutolewa kwa wasichana hao nchini kote Aprili mwaka huu - 2024.

Ilipoanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2014, ilitolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 pekee, lakini baadaye mwaka 2018, serikali iliongeza wigo na kujumuisha wasichana wenye umri wa kuanzia miaka tisa.

“Tuliamua kuwajumuisha wasichana wenye umri kuanzia miaka tisa kwa sababu tulibaini kuwa nao wanaathirika na tatizo hili. Aprili mwaka huu tuliendelea na kampeni hii ambayo imeonyesha mafanikio makubwa, tumetumia mabilioni ya fedha kuifanikisha

na hakika tumevuka lengo,” amesema Gadau.

Anasema uelewa mdogo miongoni mwa wanchi ilikuwa changamoto kubwa waliyokumbana nayo wakati wa utekelezaji wa kampeni hiyo.

“Wazazi wengi wa watoto waliokuwa wakisoma kwenye shule za bweni walikataa watoto wao kupewa chanjo, ukienda kwenye shule unaambiwa wazazi hawataki watoto wao wachanjwe.”

“Tulipata changamoto hasa baada ya kuwainigiza watoto wenye miaka kuanzia tisa kwenye kampeni ya chanjo, wazazi wengi waliogopa na kudhani kwamba hiyo ilikuwa chanjo mpya...”

“Tulipoendelea kutoa elimu, hasa kwa kuvitumia vyombo vya habari, na hamasa nyingine, ndipo walielewa,” amesema Gadau.

Saratani hiyo inaelezwa na wataalamu wa afya kuwa hushashambulia seli au chembechembe zilizomo ndani ya ngozi laini inayozunguka shingo ya kizazi.

Saratani hiyo huwapata zaidi watu wanaoanza kufanya ngono katika umri mdogo, uvutaji wa sigara, kuwa na wapenzi au kujamiiana na mtu mwenye wapenzi wengi.

Dalili ambazo zinaweza kujitokeza wakati ugonjwa upo katika hatua za mwisho ni kutokwa na damu isiyo ya hedhi, kutokwa na damu ukeni baada ya kujamiiana, kutokwa damu ukeni kwa wanawake waliokoma

hedhi na kutoka matone ya damu au damu kipindi ambacho siyo cha hedhi.



Ogopeni wanaohoji uenyekiti wa Mbowe - Dkt. Slaa

Na Hellen NGOROMERA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, amepewa sifa kwa kuwa imara, asiyeyumba na mwenye uthubutu kukabili “mawimbi makubwa ya kiasiasa.”

Sifa hizo zimewekwa wazi na aliyekuwa katibu mkuu wa chama hicho, Dkt. Wilbrod Slaa, huku akibainisha kuwa wanaohoji uenyekiti wa Mbowe ni “watu wabaya.”

Akizungumza katika mahojiano na Clouds Radio hivi kribuni, Dkt. Slaa amesema kuwa kwa mujibu wa katiba ya chama hicho cha upinzani, nafasi ya uenyekiti haina ukomo.

“Ukomo wa nafasi hii tuliundoa wakati mimi nikiwa Chadema, na tulifanya hivyo kwa makusudi na kamwe sijawahi kujuta kufanya hivyo.

“Hiyo lugha ukiisikia kwamba Mwenyekiti Mbowe amekaa muda mrefu, hao watu ndio wabaya wake,” akasema Dkt. Slaa ambaye amebainisha kuwa shinikizo la kutaka Mbowe aachie ngazi ni la kisiasa zaidi.

Akifafanua, amesema wakati huo ilikuwa ni vigumu kumpata mwenyekiti wa chama cha upinzani mwenye ujasiri na moyo wa kujitolea.

Akasema ndio maana walipompata Mbowe na kubaini kuwa ni mtu ambaye anaweza kujitolea bila woga kukiendeleza chama hicho, waliamua kuondoa ukomo wa nafasi hiyo ili kumpa uhuru zaidi wa kuwatumikia Watanzania kupitia Chadema.

Dkt. Slaa, ambaye aliwahi kuwa balozi wa Tanzania nchini Sweden, amemsifu Mbowe kwamba ameutendea haki uamuzi wa kuondoa ukomo wa nafasi hiyo kwani anachokifanya kimeimarisha zaidi Chadema na upinzani nchini.

Hata hivyo, Dkt. Slaa amesema kutokana na kazi nzuri ambayo imefanywa na Mbowe, hivi sasa Chadema imejiunga kiasi kuwa hata suala

la ukomo wa uenyekiti ukirejeshwa halitakuwa tatizo tena.

Hivi karibuni Mbowe mwenyewe alinukuliwa akisisitiza kuwa yeye ni mwenyekiti wa Chadema kwa mujibu wa katiba ya chama hicho na kwamba endapo wanachama wataamua aondoke, basi atafanya hivyo.

Kuhusu sakata la Mpina

Akizungumza kuhusiana na suala la Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina, ambaye aliadhibiwa kutohudhuria vikao 15 vya Bunge, alisema mbunge huyo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) alionewa.

Dkt. Slaa alidai kuwa Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson na wabunge, hawakumtendea haki Mpina kwa sababu aliadhibiwa bila kufuata utaratibu wa kibunge.

Dkt. Slaa anaamini kuwa Mpina alikuwa sahihi kwa yale aliyoyasema na kuyafanya na Bunge likakosea kumwadhibu.

Alisema inavyoonekana kulikuwa na njama za kumwadhibu Mpina na ndio maana hata suala lake lilingizwa kinyemela bungeni bila ya kuwepo kwenye orodha ya shughuli za Bunge za siku hiyo (order paper).

“Unakumbuka kuwa hata hoja ilipokuwa inajadiliwa mwanzoni, Spika alisema amepokea majina ya watu watano, sasa kama hoja haikuwepo kwenye order paper hao watu walijua?” alihoji Dkt. Slaa.



Dkt. Willbrod Slaa

Barua za Wasomaji

Magari misafara ya rais yapunguzwe

Mhariri,

RAIS Samia Suluhu Hassan, anafanya kazi nzuri, anahangaika huku na kule kuhakikisha kuwa “vinana wake” tunaishi vyema na kufurahia uhuru wa Tanzania.

Katika kutekeleza majukumu yake, Rais Samia lazima asafiri, atembelee huku na kule, ili kupata picha ya maisha ya watu anaoongoza, lakini pia kuzungumza na wananchi na kusikiliza kero zao.

Kitu kimoja kinachonipa shida, ni utitiri wa magari ya msafara wa Rais Samia anapokuwa anafanya ziara zake mikoani.

Idadi ya magari ni kubwa mno, kiasi kwamba magari yanaweza kufika hata 150, haya yote yakiongozana na kiongozi huyo wa nchi.

Nina uhakika kwamba gharama za magari hayo kutembea, ikiwamo madereva, mafuta na mambo mengine yanayohusika ili gari lisonge, zinabebwa na serikali.

Sasa naomba Ikulu na taasisi zingine zinazohusika kupanga mipango ya safari za rais, ipunguze idadi ya magari ili gharama zisiwe kubwa sana na fedha hizo zibaki kusaidia ustawi wa maeneo mengine.

Mwananchi,
0774124369

Je, ukuu wa Marekani unafikia mwisho?

Mhariri,

NATAMBUA kuwa kupitia gazeti lako naweza kupata majibu ya swali langu kuhusu ukuu wa Marekani katika mawanda ya usalama, uchumi na teknolojia unafika ukomo?

Nauliza hivyo kwa kuzingatia matumiko ya kuogofya ya hivi karibuni kwa mgombea urais, Donald Trump kushambuliwa, wananchi huku kulalamikia maisha magumu na kwamba teknolojia yote iliyokuwa huko Marekani, sasa inatokea China.

Je, tuamini sasa Marekani inashindwa?

Kisinzagezi,
Morogoro.

Uwekwe utaratibu mzuri kwa wateja Wizara ya Ardhi

Mhariri,

KAZI nzuri inayofanywa na gazeti lako, hakika inapaswa kupongezwa na ikiwezekana kusaidiwa kifedha na wapenda maendeleo wote, ili Pambazuko liendeleo kudumu.

Lipo jambo moja linalokera na kukatisha tamaa wateja wengi wa Wizara ya Ardhi, Nymba na Maendeleo ya Makazi, pale ofisi ya kamishna ya kuchukua hati, Kivukoni, Dar es Salaam.

Katika ofisi hiyo, wateja ni wengi mno ambao hujazana ndani ya chumba kimoja, huku wakisubiri huduma kutoka kwa watendaji.

Wahudumu wanafanya kazi nzuri, lakini ni kama wanahemewa na idadi kubwa ya wateja “wanaolundikwa” ndani ya chumba hicho.

Sasa kwanini, kusiwekwe utaratibu wa kuruhusu watu wasiozidi kuingia kwa mara moja na baada ya kuhudumiwa wakaondoka?

Na kwa wale ambao hati zao ama nyaraka zingine bado hazijawa tayari wakaelezwa hivyo na kuondoka ili kutoa nafasi kwa wengine?

Ni hatari sana kwa afya za wateja na mbaya zaidi kwa watendaji kwa kuwa wanakumbana na mgandamizo mdogo wa hewa, hata kama kuna viyoyozi.

Kuendelea kujaza watu ndani ya chumba hicho, kuachwe sasa na waingie wateja wachache zaidi ili kulinda afya na kuboresha utendaji.

Juma Othman Masoud,
Ilala, Dar es Salaam.

NUKUU



Usinipime mimi kwa mafanikio yangu ya sasa, bali chunguza ni mara ngapi nimeanguka, kuinuka na kuendelea na mapambano.
Nelson Mandela





Nape, Makamba 'OUT'

Inatoka Uk. 12

Mbarouk Nassor Mbarouk ambaye atapangiwa kituo cha kazi; Deus Clement Sangu, ameteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Dennis Lazaro Londo, ameteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki. Londo anachukua nafasi ya Stephen Lujwahuka Byabato (Mb.) ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Eliakim Chacha Maswi, ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Kabla ya uteuzi huu Maswi alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Mary Gaspar Makondo, ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma. Kabla ya uteuzi huu Makondo alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Makondo anachukua nafasi ya Rehema Sefu Madenge ambaye amestaatu.

Kiseo Yusuph Nzowa, ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro. Kabla ya uteuzi huu Bw. Nzowa alikuwa Afisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais –

Ikulu.

Musa Haji Ali, ameteuliwa kuwa Balozi. Kabla ya uteuzi huu Ali alikuwa Afisa Mwandamizi, Ofisi ya Rais - Ikulu; Louis Peter Bura, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Chato. Bura anachukua nafasi ya Said Juma Nkumba ambaye amepangiwa majukumu mengine.

Kemirembe Rose Lwota, amehamishwa kutoka Wilaya ya Manyoni kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Serengeti.

Dkt. Vincent Biyegela Mashinji, amehamishwa kutoka Wilaya ya Serengeti kwenda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Manyoni.

Dkt. Maulid Suleiman Madeni, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

Afraha Nassoro Hassan, amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Hassan anachukua nafasi ya William Anyitike Mwakalambile ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Dennis Kwame Simba, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA). Kabla ya uteuzi huu Simba alikuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Uvuvi Tanzania (Tafico).

Samia avunja rekodi Usalama wa Taifa

Inatoka Uk. 14

hatarishi na usalama katika uchaguzi, hivyo inawezekana mabadiliko yanahusisha kulivusha taifa katika uchaguzi ujao.

Mabadiliko yaliyofanyika

Januari 3, 2023 - Rais Samia alimteua Said Hussein Massoro kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa, akichukua nafasi ya Diwani Athumani aliyeongoza tangu mwaka 2019.

Agosti 28, 2023 - Rais Samia alimuapisha Balozi Ali Idi Siwa kuongoza idara hiyo akichukua nafasi kutoka kwa Said Masoro aliyeongoza kwa miezi minane.

Julai 11, 2024 - Rais Samia alimuapisha Suleiman Abubakar Mombo kuwa "kiranja" wa idara hiyo akichukua nafasi ya Balozi Ali Idi Siwa ambaye amestaafu. Kabla ya uteuzi huo, Mombo alikuwa Ofisa Mwandamizi Ofisi ya Rais Ikulu.

Mombo anafanya idadi ya walioshika wadhi-

fa wa wakurugenzi wakuu wa idara hiyo kufikia wanne tangu Rais Samia alipoapishwa kushika madaraka hayo Machi 19, 2021.

Wakurugenzi Usalama wa Taifa tangu Uhuru Tangu nchi kupata uhuru Idara ya Usalama wa Taifa imekuwa na wakurugenzi 12, ambao ni Emilio Mzena - 1961 hadi 1975 (miaka 15), Dkt. Lawrence Gama 1975-1978 (miaka minne), Dkt. Hassy Kitine 1978-1980 (miaka mitatu), Balozi Augustine Mahiga 1980-1983 (miaka minne), Luteni Jenerali Imran Kombe; 1983-1995 (miaka 12), Apson Mwang'onda; 1995-2005 (miaka 10), Othman Rashid; 2005-2016 (miaka 10) na Dk Modestus Kipilimba; 2016-2019 (miaka minne).

Wengine ni Diwani Athumani; 2019 -2023 (miaka mitano), Said Hussein Massoro; Januari - Agosti 2023 (miezi minane), Balozi Ali Idi Siwa; 2023- Julai 2024 (Miezi 11), Suleiman Mombo; Julai 11, 2024 hadi sasa.

Matukio katika picha Rais Samia na Machifu



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika picha ya pamoja na Machifu kutoka mikoa mbalimbali nchini, Ikulu Chamwino Dodoma. Julai 20, 2024. (Picha zote na Ikulu)



Rais Samia Suluhu Hassan akiwahutubia machifu Ikulu Chamwino Dodoma.



Mmoja wa Machifu akimsikiliza Rais Samia.



Rais Suluhu Hassan akisalimia baadhi ya Machifu Ikulu Chamwino Dodoma.



Hitilafu Microsoft ‘yasimamisha dunia’

Washington, MAREKANI

IMETHIBITIKA kuwa sasa dunia inaweza “kusimama” endapo kutatokea hitilafu au mparaganyiko kwenye mifumo mahsusi ya kuendesha shughuli za uzalishaji, usafiri na usalma.

Shughuli hizo ni pamoja na usafiri wa anga, mawasiliano, habari, huduma za kibenki, uzalishaji wa kibiashara, uendeshaji wa serikali na usalama.

Hali hiyo imethibitika Ijumaa – Julai 19, baada ya kutokea kwa hitiafu katika mifumo ya mawasiliano wa Microsoft Cloud, inayounganisha dunia.

Awali, ilidhaniwa kuwa hitilafu hiyo iliyootokea mapema siku hiyo ilisababishwa na shambulio la kigaidi, lakini wataalamu wakathibitisha saa chache baadaye kuwa ilikuwa ni hitilafu ambayo haikusababishwa na magaidi.

Mashirika makubwa ya ndege, benki na shughuli nyingi za kiserikali duniani kote ziliathiriwa na hitilafu hiyo na kusababisha kuahirishwa kwa safari nyingi za ndege, kufungwa na benki na kukosekana kwa huduma za matangazo ya radio na runinga, halikadhalika huduma zinazotolewa na taasisi za umma katika maeneo

mengi duniani.

Mashirika makubwa ya ndege nchini Marekani yakiwemo Delta, United na American Airlines pamoja na maeneo mengine duniani, yalilazimika kusitisha safari zake kutokana na hitilafu za mawasiliano kwenye viwanja vya ndege.

Mamilioni ya abiria duniani kote waliathirika na hatua hiyo huku wengi wakilazimika kushinda katika viwanja vya ndege kwa muda mrefu baada ya safari zao kusitishwa.

Mara baada ya tukio hilo, wataalamu wa kampuni ya Microsoft walisema kuwa wameanza uchunguzi wa suala hilo na muda mfupi baadaye wakatoa taarifa kuwa chanzo cha tatizo hilo kilikuwa kimefahamika na juhudi za kutatua zilishaanza.

“Mapema leo asubuhi (Ijumaa iliyopita) suala la kiufundi kwa upande wa mtoa huduma liliathiri mashirika kadhaa likiwemo mashirika ya ndege, lakini tumeweza kuanza shughuli zetu tena...”

“Tunaomba radhi kwa wateja wetu kwa matatizo yaliyojitikeza,” liliandika shirika la ndege la American Airlines katika taarifa yake.

Shirika la usimamizi wa safari za anga nchini

Inaendelea Uk. 23



Je wajua



Kinyonga anaweza kuangalia vitu viwili kwa kutumia macho yake mawili, yaani jicho moja linaweza kuwa linaangalia mbele na jicho lingine linaangalia nyuma. Hakuna mnyama mwingine mwenye uwezo huu.



Bilionea Aliko Dangote aliwahi kutoa kiasi cha dola milioni 10, (zaidi ya shilingi bilioni 25) benki na kurudi nazo nyumbani ili aone zinafananaje na kwa wingi gani kisha asubuhi alizirejesha tena benki. Alitaka kujua ubilionea unafananaje

Hitilafu Microsoft 'yasimamisha...

Inatoka Uk. 22

Marekani, FAA, lilisema kuwa hitilafu hiyo ilisababisha kusitishwa kwa safari zote za anga nchini humo.

Tatizo lilivyoanza

Kampuni kubwa ya teknolojia ya Marekani, Microsoft ilisema kuwa hitilafu katika mifumo ya 'Azure Cloud' ilizima ghafla na kuwaathiri baadhi ya wateja katika baadhi ya maeneo ya Marekani.

Ilidaiwa kuwa upo uwezekano kwamba moja ya kampuni zilizokuwa zikirekebisha mfumo wa mawasiliano, CrowdStrike ilifanya jambo bila kujua na kusababisha kusimama kwa baadhi ya shughuli zinazoendeshwa kwa mifumo ya mawasiliano.

CrowdStrike ni moja ya kampuni za teknolojia inayotumiwa na Microsoft kutoa huduma za usalama mtandaoni kwa wateja wake, ikijikita kwenye masuala ya kutambua na kuzuia udukuaji.

CrowdStrike ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusiana na hitilafu katika mifumo yake ndani ya mfumo wa uendesha-ji wa Microsoft Windows.

Wahandisi wa kampuni hiyo waliingia kazini mara moja kukabiliana na hitilafu hiyo na kubaini eneo ambalo lilisababisha hitilafu hiyo.

Ili kukabiliana na hali hiyo kampuni ilitoa maelekezo kwa wateja wake kuzima na kuwasha upya vifaa vyao, na baada ya kurekebisha hitilafu.

Moja kati ya majukumu am-

bayo CrowdStrike inayafanya ni kutoa huduma za usalama mtandaoni kwa kuwasaidia wateja wake kugundua na kuzuia mashambulizi ya wadukuzi.

CrowdStrike ilijipatia umaarufu kwa kuchunguza uduku uliofanywa na Urusi kwenye kompyuta za Kamati Kuu ya Chama cha Democratic wakati wa uchaguzi wa mwaka 2016 nchini Marekani.

Hekahaka


Hitilafu iliyotokea jana ilithiri pia huduma za afya nchini Uingereza kama ilivyoripotiwa na serikali ya nchi hiyo kupitia wizara yake ya afya (NHS). "NHS inafahamu kuhusu tatizo la mtandao. Tumechukua hatua madhubuti kukabiliana na tatizo hilo kwa kuhakikisha hakuna huduma zitakazoathirika," ilisema NHS.

Kwa upande mwingine, mfumo wa kuhudumia wateja katika mfumo wa usafiri Marekani nao uliathirika na tatizo hilo, ingawa huduma za safari za mabasi na treni hazijaathiriwa.

Viwanja vingi vya ndege barani Ulaya na Asia navyo vili fungwa na safari kuahirishwa kutokana na hitilafu hiyo.

Baadhi ya viwanja vikubwa vya ndege vilivyoathirika ni

Gatwick cha London, uwanja wa ndege wa Berlin, Ujerumani, Schiphol jijini Amsterdam nchini Uholanzi, Edinburgh huko Scotland na viwanja kadhaa nchini Hispania na India.



Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL



Nilipata taabu kumwelewa Nape Nnauye

ALIYEKUWA Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alichafua hali ya hewa.

Wiki iliyopita alipokuwa akizungumza mkoani Kagera, aliutangazia umma kuwa yeye ni bingwa wa kupindisha matokeo na matakwa ya wapiga kura.

Kwa kujiamini alimweleza Mbunge wa Bukoba Mjini, Stephen Byabato, kuwa anaweza kumfundisha mbunge huyo mbinu halali, nusu halali na haramu za kushinda uchaguzi.

Alimweleza mbunge huyo na watu waliokuwa wanamsikiliza, kuwa matokeo ya uchaguzi hayategemei tu idadi ya kura zilizomo kwenye sanduku la kura, bali nani anazihesabu.

Kwa mujibu wa Nape, njia za kupata matokeo ya aina hizo, zinaweza kutumika kwa sababu baada ya kuzitumia, unaweza kumomba Mwenyezi Mungu akusamehe kwa ulichokifanya.

Hiyo ndiyo kauli ya Nape ambaye miaka kadhaa iliyopita, wakati akiwa Msemaji wa CCM - mwaka 2015, aliwahi kukaririwa akisema chama chake kiko tayari kushinda uchaguzi hata kwa 'bao la mkono' pindi kitakapoona mazingira ya uchaguzi kinaoshiriki ni magumu.

Nilimfikiria sana Nape. Nikafikiria cheo alichokuwa nacho. Nikafikiria wadhifa wake. Nikafikiria hadhi yake. Nikafikiria sana kauli aliyotoa na, ninashindwa kuelewa alikuwa anataka kupeleka ujumbe wa aina gani kwa Watanzania wanaotarajia kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye mwaka huu.



Sijaelewa alikuwa anataka Watanzania waelewe kitu gani wakati wanajiandaa kushiriki Uchaguzi Mkuu mwakani.

Mwenyewe baadaye anasema kuwa alikuwa anafanya utani, lakini anapaswa kuelewa kuwa hicho anachokiita au kukiona kama utani, ni uchochezi wa hali ya juu.

Kwa kauli yake hiyo, ametuambia Watanzania kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambacho kinatamba kujijengea heshima nchini na duniani kote, hakifuati Katiba wakati wa uchaguzi unapofanyika.

Nape anataka kuwaambia Watanzania na vyombo vyote vya ulinzi na usalama, kwamba Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) pamoja na Katiba ambayo ndiyo msingi wa chaguzi zote za kisiasa nchini, havina maana.

Nape anataka kukiambia chama chake, anataka kuiambia vyama vya upinzani na Watanzania kwa ujumla wao kwamba sheria na kanuni za uchaguzi siyo lolote wala chochote kwa sababu zinaweza kuvunjwa wakati wowote ili kuhlalisha matokeo haramu yanayoweza kumuweka mtu madarakani hata kama wanchi wamemkataa!

Aidha, inaonekana Nape siyo muumini wa kutii sheria na taratibu zilizowekwa na mamlaka, bali yeye ni mtaalamu wa kufanikisha anachokitaka kwa njia haramu huku akitegemea kutubu na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu.

Kauli ya Nape imefanya Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua hatua ya kutengua uwaziri wake, hivyo na CCM wanatakiwa sasa kumdhibiti mwanasiasa huyo, wamuonye na ikibidi wamchukulie hatua zinazostahili.

CCM isipofanya hivyo, kuna hatari wananchi wakaiadhibu kwa kosa na majigambo ya Nape.



Dkt. Henga: Katiba mpya itakwamua mengi



Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga (kushoto), akizungumza na Mwandishi Mkuu wa gazeti hili, Elizabeth Hombo, wakati wa mahojiano maalum ofisini kwake, jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Fidelis FELIX)

MKURUGENZI Mkuu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dkt. Anna Henga amehojiwa na Mwandishi wa Pambazuko, **Elizabeth HOMBO** kuhusu masuala mbalimbali ya Tanzania na hapa anajibu maswali aliyohojiwa...

Pambazuko: Unauonaje mwelekeo wa hali ya haki za binadamu Tanzania?

Dkt. Henga: Hali ya haki ya binadamu ina mchanganyiko kidogo. Kuna maeneo ambayo hali imekuwa nzuri, lakini kuna maeneo hali imekuwa mbaya.

Lakini, ukiangalia kwa takwimu, mwaka 2023 tumedorora kidogo kuliko mwaka 2022.

Haki za wanawake na watoto na watu wenye ulemavu zilivunjwa zaidi, haki za watoto zimevunjwa kuliko haki zote.

Ubakaji, ukatili wa kingono na uingiliwaji wa watoto kinyume na maumbile, hali imekuwa mbaya sana.

Kwa mfano, kwa hivi sasa ukatili kwa wanawake, hasa ubakaji, vipigo na mauaji ya wenzazametokea kwa wanawake kwa asilimia 90, huku wanaume ikiwa ni asilimia 10 tu.

Pambazuko: Nini maoni yako kuhusu usalama wa watu wenye ulemavu wa ngozi nchini?

Dkt. Henga: Kuhusu albino kwa kweli Tanzania tunatia aibu sana kimataifa, kwa sababu huwezi kutegemea viungo vya binadamu mwenzako eti ili ushinde uchaguzi, ufanye biashara ikae vizuri.

Kama ingekuwa hivyo, basi watu wenye ualbino wenyewe ndio wangukuwa matajiri au viungo wakubwa kwa sababu wana viungo vyao na wanatembea navyo.


Kutumia viungo vya mwenzako ni imani potofu, ya zamani na isiyokuwa na maana kabisa. Naishauri sana jamii inayofanya hivyo iachane na imani potofu... tufanye kazi kwa bidii tutapata fedha na mafanikio.

Kama ni mwanasiasa fanya siasa kwa bidii usaidie watu wa jimboni kwako, saidia jamii inayokuzunguka watakupa tu kura.

Kuwa na ilani nzuri ya uchaguzi, itakusaidia kupata kura na siyo kutegemea viungo vya albino.



Ana kwa Ana



Dkt. Henga: Katiba mpya itakwamua mengi

Inatoka Uk. 25

Pambazuko: Kwa uzoefu wako nini matarajio yako katika siku zijazo katika eneo hili la haki za binadamu?

Dkt. Henga: Matarajio yangu mimi ninasubiri Katiba mpya.

Tukipata Katiba ambayo ina uhakika kulin-da haki za binadamu, ni rahisi kutunga sheria mbalimbali za masuala haya.

Tumeahidiwa kwamba mwaka 2026 angalau tutakuwa na Katiba mpya kupitia mchakato mpya au tutauendeleva ule wa iliyokuwa Tume ya Jaji Joseph Warioba.

Lakini, pia kwenye haki za makundi tuki-pata sheria ya kupinga ukatili wa kijinsia am-bayo waziri ametuahidi, basi tutakuwa tumefika pazuri kidogo kuhusiana na ukatili wa kingo-no kwa wanawake na watoto pamoja na ukatili mwingine.

Pambazuko: Unazungumziaje hali ya siasa hapa nchini kwa sasa?

Dkt. Henga: Hali ya kisiasa angalau imekuwa bora kidogo ingawa siyo sana, lakini imeboreka kidogo kwa sababu kwa sasa angalau tunaweza kupata maoni kidogo na vyombo vingi vya habari vimefunguliwa na tunaweza kutoa maoni yetu.

Pambazuko: Umeongoza LHRC kwa kipindi

kirefu, ni mazingira gani na changamoto ambayo umekutana nayo kikazi ambayo huwezi kuyasahau?

Dkt. Henga: Nimeongoza LHRC kwa miaka sita sasa, lakini changamoto kubwa ni kwamba kazi ni nyingi.

Kazi ni kubwa sana ya kutetea haki za watu na unakuta LHRC ndiyo wenyewe tu ambao tunatetea haki za binadamu, wapo na wadau wengine, lakini sisi tunafanya kwa ukubwa nchi nzima.

Tunafanya kwenye maeneo yote ya haki za binadamu kwa hiyo mahitaji ni makubwa wakati mwingine kuna watu usipowatetea na jambo limekupita, hujaliona, basi inakuwa ugomvi mkubwa.

Unakuta watu wanalalamika kwanini ham-jatutetea? Hadi kwenye mitandao ya kijamii, mjadala unaibuka kwamba kwa nini hamjasema kuhusu suala hili.

Watu wanataka sisi tuseme neno, wanaona neno letu ni dawa na tukisema kitu kinabadi-lika, kwa hiyo kila mtu anatutarajia.

Tunamshukuru Mungu tunapambana zaidi na zaidi.

Kitu ambacho huwa sikisahau mara nyingi ni pale ambapo tumemsaidia mtu na baadaye akapata haki yake, akafurahi.

Lakini kinyume chake tumesaidia mtu halafu baadaye akaacha kesi yake, kama ni mwana-mke akadhurika zaidi na pengine kufariki dunia au kukata tamaa mwishoni.

Kwa hiyo hili linatumiza zaidi.

Pambazuko: Unajivunia nini katika uongozi wako LHRC?

Dkt. Henga: Ninajivunia kwamba kwa sasa LHRC imekuwa kimbilio la wanyonge.

Najivunia kwamba nina timu imara inayofa-nya kazi ya utetezi kwa haraka na kwa wakati na tunaweza kusema kwamba LHRC ni shirika linalotetea watu wengi zaidi na kila siku wana-saidiwa watu zaidi ya 100.

Pia tuna App yetu ya haki kiganjani. Kila siku inasaidia na kuhudumia watu zaidi ya 40 ambao wanaweza kupata haki zao.

Pambazuko: Unauzugumziaje uongozi wa ser-ikali ya awamu sita chini ya Rais Samia Suluhu

Inaendelea Uk. 27

Dkt. Henga: Katiba mpya itakwamua mengi

Inatoka Uk. 26

Hassan ukilinganisha na ule wa awamu ya tano?

Dkt. Henga: Kwa uongozi wa awamu ya sita kwanza tunafarijika tumebarikiwa na rais wa kwanza mwanamke.

Ni nchi chache za Afrika ambazo zimebarikiwa kuwa na rais mwanamke.

Kitaaluma inaitwa 'feminine type of leadership' yaani aina ya uongozi wa kike ambapo anaweza kukusanya mawazo yote ya watu na kuyafanyia kazi.

Ingawa hawezi kuyafanyia kazi yote, lakini anaweza kuyakusanya na kuyasikiliza.

Na kwa mara ya kwanza tunaweza kumwalika rais kwenye matukio ya haki za binadamu na akaja, akatoa hotuba yake kwa hiyo ni kitu ambacho ni kizuri na tunashukuru kwa hilo.

Kitu kingine ambacho naweza kulinganisha ni kuwa awamu ya tano ilikuwa haisikilizi maoni ya watu na tulikuwa tunaelekea kutumbukia shimoni kwa masuala ya demokrasia na ya haki za binadamu.

Lakini, sasa angalau Rais Samia alipokuja amefungulia mikutano, ammeokoa nchi na sasa amewaacha wanasiasa wanaongea wanam-challenge (wampe changamoto) lakini amekuwa mstahimilivu na mvumilivu.

Pambazuko: Unaionaje hali ya demokrasia nchini?

Dkt. Henga: Hali ya demokrasia kwa sasa iko kwa vitendo kuliko sheria kwa maana kwamba sheria zilizopo haziendeni na hali iliyopo.

Angalau kwa mambo machache kama sera za jinsia kwenye vyama, kutambua ukatili wa kijinsia kama kosa ndani ya uchaguzi na vitu kama hivyo, lakini haijaleta mabadiliko makubwa kama ambavyo tulitegemea, ndiyo maana tunasema Katiba irekebishwe.

Kwa upande mwingine, kama nilivyosema awali, angalau watu wanakutana wanafanya siasa hawajafungiwa kama wakati ule.

Lakini inatakiwa sheria irekebishwe kuwafanya wawe huru zaidi ili mtu akishindwa kwenye uchaguzi, basi aseme kweli kashindwa kwani hakuna anayebanwa.



Dkt. Anna Henga

Pambazuko: Wakati wa uongozi wa awamu ya tano, taasisi nyingi zenye mwelekeo kama wa LHRC zilipitia changamoto nyingi ikiwemo kunyimwa leseni na kuzuiwa au kufungiwa. Je, hali ilikuwaje kwa LHRC?

Dkt. Henga: LHRC hatukufungiwa, lakini tulikuwa na hekaheka nyingi za kunyiwa vibali vya kufanya kazi, lakini sasa hivi mambo yamebadilika na tunapewa vibali.

Kwa mfano, kwenye uchaguzi unaokuja, tunaendelea kutoa elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia kwa mujibu wa sheria.

Tutaendelea kufanya kazi ya uangalizi wa haki za binadamu na suala la uangalizi ni la kisheria kabisa kabisa.

Ukishamtoa tu mwangalizi au ukatoa waangalizi ambao ni strong (mwenye nguvu) kama LHRC, uchaguzi wako lazima utakuwa wa shaka.

Lakini ukiwaweka wale ambao ni strong na wanaojifunza, basi itapendeza zaidi.

Safari hii naona tumejifunza na tunaendelea kupewa vibali na tunafanya kazi ya kuangalia na pia kushauri kwa sababu nia yetu siyo tukosoe, bali ni ili tutoe ushauri bora zaidi wa namna ya kufanya uchaguzi kuwa bora zaidi.

Pambazuko: Unauonaje mwenendo wa Bunge la sasa, unadhani linawakilisha wananchi na kusimamia serikali ipasavyo?

Ana kwa Ana

Dkt. Henga: Katiba mpya itakwamua mengi

Inatoka Uk. 27

Dkt. Henga: Bunge la sasa naweza kusema changamoto yake kubwa ni kwa sababu halina sauti mbadala. Asilimia kubwa ni chama kimoja.

Kwa hiyo, hata wakicharurana, wakimaliza hawawezi kusema watakataa muswada kwa sababu wana caucus (kambi) yao ya chama na ndiyo Bunge.

Kwa hiyo ni ngumu kupata mawazo mbadala tofauti na mabunge ya zamani yalikuwa na sauti tofauti tofauti atazungumza Chadema, ACT-Wazalendo, TLP... kwa hiyo unapata ladha tofauti.

Siasa ni ushirikishwaji wa watu mbalimbali. Nasihi kwenye uchaguzi huu tuwe na wabunge wa vyama tofauti ili tuwe na hamasa kwenye Bunge.

Bunge hili la chama kimoja hata likifanya vizuri, haiwezi kuonekana kuwa haki imetendeka watu watasema si hao hao CCM!

Ni vizuri sasa kuwe na sauti mbalimbali, mimi ni mtu wa asasi za kiraia na sina chama wala sitakiwi kuwa na chama, lakini nafurahia kuona kwamba vyama vingi vinashirishwa kama iinavyosema katiba yetu.

Pambazuko: Hujawahi kupata vitisho vyo vyote kutoka kwa wasiopendekezwa harakati zako?

Dkt. Henga: Vitisho vipi

Pambazuko: Vya namna gani?

Dkt. Henga: Wavunjaji haki wengine wanatumia message (ujumbe) na kupiga simu wakitishia kuwa nache ninachokifanya.

Pambazuko: Kitisho kipi ambacho pengine kiliwahi kukutisha zaidi?

Dkt. Henga: Aaah nimeshakomaa sasa vyote naona ni kawaida tu.

Pambazuko: Unadhani yanayotokea Kenya yanaweza kutokea na hapa Tanzania?

Dkt. Henga: Yatakuja tu ingawa kwetu social economic content (misingi ya kijamii na kiu-chumi) ni tofauti kidogo kwa sababu Tanzania tunaishi kijamaa, lakini Kenya ni wanaishi kibepari.

Tayari Uganda pia imeanza, wameanza kundesha kampeni ya Museveni must go (Museven aondoke).

Ila sasa sisi kinachotusaidia ni udugu, tunaiishi kigudu zaidi, Kenya wanaishi kibepari.

Mfano sisi Tanzania hatumiliki ardhi tofauti na Kenya, huko ukipata ardhi inakuwa ni ya kwako, hapa kwetu ni tofauti.

Tanzania ardhi ni ya serikali chini ya usimamizi wa rais, ndiyo maana mara nyingi unakuta watu wanahamishwa kwa ajili ya kupisha miradi fulani labda.

Sasa Kenya hawa vijana maarufu Gen Z hawana ardhi, hawana pa kukaa, hawana ajira na kule hakuna mashamba labda ya kulima kama Tanzania hivyo wale Gen z hawana cha kupoteza.

Sasa tatizo lilipo hapa kwetu watu hawajui masuala ya haki. Wakenya wao wamejikita kwenye elimu zaidi kutokana na madhila waliyopitia.

Hapa Tanzania unakuta wakati mwingine sisi tunasaidia kupata haki zao lakini wanatupiga vita.

Pambazuko: Unadhani kama taifa kwenye masuala ya haki tumepiga hatua au tunarudi nyuma?

Dkt. Henga: Tumekaa. Hatuendi mbele tunapiga hatua moja ya konokono.



Bunge la Tanzania, Dodoma



Utata dampo kukutwa miili ya wanawake



Rais wa Kenya, William Ruto.

Na Julius MKAMBI, Nairobi

IDARA ya Upelelezi Makosa ya Jinai (DCI) nchini Kenya imetupia lawama na wananchi kufuatia kugundulika kuwepo miili ya wanawake.

Pamoja na kwamba idadi hiyo imekuwa ikiongezeka, baada ya ya kazi ya kufukua, inakadiriwa kuwepo kwa miili zaidi ya 10.

Mbali na miili hiyo iliyokutwa ikiwa imekatwakatwa baadhi ya viungo na kuharibika, pia kume kuwepo mifupa ya binadamu katika dampo la Kware eneo la Mukuru Kwa Njenga, jijini Nairobi.

Siku moja baada ya kugundulika kwa miili hiyo, Rais William Ruto aliwahakikishia Wakenya kwamba wahusika wote wa tukio hilo la kutisha watakatwa na kushitakiwa.

Tayari DCI imetangaza kumkamata Collins Jomaisa waliyemtaja kuwa mhusika mkuu kufuatia kukiri kuwauwa wanawake 42 tangu mwaka 2022 ikiwemo mkewe.

Mkurugenzi wa DCI, Mohammed Amin, amesema mshukiwa huyo alieleza kwamba alichochewa kuwa muuaji katili, baada ya kumuanzishia mkewe biashara, lakini akashindwa kuiendeleza na kusababisha kusambaratika.

Ameongeza kuwa mshukiwa alimsaidia mkewe kuanzisha tena biashara nyingine ambayo pia ilisambaratika na hapo ndipo alipatwa na hasira na kuishia kutoa uhai wa mkewe.

Wapelelezi wanaendelea kuchunguza madai ya mshukiwa ya kumuua mkewe na kumkatakata vipande vipande kabla ya kumtupa kwenye dampo la Kware.

“Inaonekana ni mtu aliyejawa na kisasi na chuki na alikuwa na upendeleo maalumu kwa wanawake kulingana na alivyotuaambia,” amesema bosi wa DCI Amin.

Jomaisa alipofikishwa mahakamani wiki iliyopita alijitetea kwamba alilazimishwa kukiri kuwauwa wanawake 42 na polisi.

Licha ya maelezo ya DCI, bado yapo maswali yanayohitaji majibu, ikiwemo ni vipi mtu mmoja, tena ndani ya miaka miwili amewauwa wanawake 42 kisha kuwakata vipande vipande, miili yao akaweka kwenye gunia na kutupa kwenye dampo bila hata Jeshi la Polisi kugundua?

Jirani na dampo hilo kuna Kituo cha Polisi.

Awali kabla ya kukamatwa kwa mshukiwa huyo, DCI Amin alisema katika uchunguzi wao wanalenga kubaini kama tukio hilo linalohusishwa na ushirikina, mauaji ya kikatili au madaktari walaghai waliojitosa kwenye shughuli za uhalifu.

Mtu mmoja kutoa uhai kikatili wanawake 42 ndani ya miaka miwili, je, alikuwa anafanya hivyo pekee yake au kuna genge kubwa nyuma yake?

Je, alikuwa anawezaje kutekeleza kitendo hicho cha unyama pasipo majirani kusikia? Aliwezaje kubeba magunia yaliyokuwa na miili hadi machimboni au wapo watu walikuwa wanamsaidia?

Bado kuna utata unaozunguka sababu ya mshukiwa kugeuka ‘muuaji katili’ pale alipodai kuchukizwa na kitendo cha kumuanzishia biashara mkewe mara mbili na kushindwa kuendesha kiasi cha kusambaratika.

Je, alikuwa anatenda tukio hilo la kusikitisha maeneo gani? Kama ni kwake nyumbani, majirani hawakugundua kitu chochote kisichokuwa cha kawaida?

Lakini swali gumu ambalo DCI wanashindwa kujibu, inakuaje Collins Jomaisa anaweza kukamatwa siku moja tu baada ya kugundulika kwa miili kwenye dampo la Kware wakati wale wanaohusika na utekaji nyara na mauaji ya kiholela hawakamatwi?

Inaendelea Uk. 30

Kenya



Picha ikionesha dampo ilipotupwa miili ya wanawake sita ikiwa imekatwakatwa na kufungwa kwenye mifuko ya nailoni jijini Nairobi. (Picha na DW)

Utata dampo kukutwa miili ya wanawake

Inatoka Uk. 29

Itakumbukwa Rais Ruto aliaapa katika serikali yake hakutakuwa tena na utekaji nyara na mauaji ya kiholela, lakini matukio haya yameshamiri wakati vijana wa Gen Z walipokuwa wanaandamana wakitaka serikali iwajibike kwa ahadi walizotoa.

Licha ya Rais Ruto kukana uwepo wa utekaji nyara, Naibu Rais Rigathi Gachagua alikiri kurudi tena kwa matukio hayo ambayo yanafanyika peupe na watu ambao wanasaidikiwa ni maafisa wa kitengo maalumu cha polisi.

Kisa cha kusikitisha kilichotokea dampo la Kware kimeibua utepetevu kwenye Jeshi la Polisi kufuatia kugundulika kwa makaburi ya watu wengi katika Msitu wa Shakahola uliopo Kaunti ya Kilifi, Pwani ya Kenya.

Aprili mwaka jana - 2023, polisi walipuuza ripoti iliyowasilishwa kituoni na mwanamume moja aliye-lalamika kwamba mkewe na binti yake waliondoka nyumbani kujiunga na kanisa lililokuwa linamilikiwa na mchungaji Paul Mackenzie wakisema hayo ni mambo ya wachungaji kung'ang'aniana waumini.

Lakini taarifa zilipoanza kuzagaa kwenye vyombo vya habari, polisi walivamia shamba la Mackenzie lenye ekari 800 katika Msitu wa Shakahola na kugundua makaburi ya watu wengi na walipofukua wakapa-

ta zaidi ya miili 400.

Kwasasa Mackenzie anashikiliwa na Jeshi la Polisi akiwa amefunguliwa mashtaka ya uhalifu unaohusiana na ugaidi, mauaji na mateso ambapo Desemba mwaka jana, alihukumiwa kifungo cha miezi 12 baada ya kupatikana na hatia ya kutengeneza na kusambaza filamu bila leseni.

Tofauti ya kanisa la Mackenzi na makanisa mengine, ni kwamba katika kanisa lake, watu walilazimishwa kufunga na matokeo yake wakafa kwa njaa au kupigwa na kuuwawa walipojaribu kuondoka.


Missing Voices, kikundi cha kampeni kinachotangazia mauaji ya kiholela nchini Kenya, kiliwahi kusema kumekuwa na vifo 1,160 mikononi mwa Polisi tangu ilipoanza kukusanya data mwaka 2017, na watu 269 walilazimisha kutoweka.

Ukiacha kugundulika kwa idadi kubwa ya miili katika dampo la Kware na Msitu wa Shakahola, miili pia iliwahi kugundulika imetupwa katika Mto Yala ambapo shirika lisilo la kiserikali, Haki Africa, lilisema kutupwa kwa miili hiyo inakera na kutaka Polisi kuchunguza ili kubaini kama wao wenyewe walihusika au la katika mauaji hayo.

Hii ni baada mpigambizi Nicholas Okero Okite ambaye alikuwa anatoa maiti zisizofahamika kutoka Mto Yala kwenda mafichoni akidai kutishiwa maisha.

Kwa mujibu wa Haki Africa, Okite aliyesaidia kupatikana kwa miili takribani 26, alipokea vitisho kutoka kwa polisi na hata kunyang'anywa simu yake.

Mauji ya kiholela na visa vya utekaji nyara ni miongoni mwa vitendo ambavyo vijana wa Gen Z wana-vilaani kupitia maandamano ya kushinikiza serikali ya Rais Ruto kuwajibika.



Na Hellen
NGOROMERA



Tukutane hapa kuhusu masuala ya uhusiano

KARIBU mpenzi msomaji katika safu hii mpya ya uhusiano.

Safu hii inalenga kuibua masuala anuai kuhusu uhusiano kati ya mtu mmoja mmoja au jamii kwa ujumla.

Masuala kama ndoa, mapenzi, maadili, udugu na yanayofanana na hayo, ndiyo yatakyojadiliwa kupitia safu hii.

Imeniwia vigumu kuamua ni jambo gani mahsusi la kuanza nalo, hivyo niruhusuni katika safu hii kuanza na masuala ya jumla kuhusiana na uhusiano.

Safu inalenga kuzungumza na watu wa rika zote.

Tutazungumza kuhusu uhusiano kati ya watoto na watu wazima, tutazungumzia kuhusiana na uhusiano wa vijana na pia uhusiano kati ya watu wazima kwa kutaja maeneo machache nitakayogusia.

Kuna suala la mawasiliano katika uhusiano. Tatalianguka hilo kwa sababu kuwasiliana kwa uwazi na kwa ufanisi ni sehemu muhimu ya kuelewa hisia na mahitaji ya kila mmoja.

Pia kuna suala la uaminifu katika uhusiano. Kujenga na kudumisha uaminifu ni msingi wa uhusiano mzuri.

Kukosekana kwa uaminifu kunaweza kuleta matatizo makubwa.

Suala la heshima nadhani halihitaji maelezo marefu, kwa sababu kila mmoja anapaswa kuheshimiwa yeye binafsi, mawazo, hisia na mipango hali kadhalika.

Kimsingi, heshima ni kati ya misingi mizuri wa uhusiano.

Pia tutaangalia kuhusu utatuzi wa migogoro kwani mikwaruzano katika uhusiano, ni jambo lisilowezi kuepukwa.

Kutokana na hayo, kuna haja ya kujua jinsi ya kutatua migogoro kwa njia ya amani ni muhimu.

Pia kuna suala la kusaidiana katika nyakati ngumu na kusherehekea mafanikio kama sehemu

muhimu kwa kujenga uhusiano imara.

Kuelewa na kuheshimu mipaka ya kila mmoja ni muhimu ili kuzuia kuingiliana na kuheshimu nafasi za kibinafsi.

Kwa kuwa uhusiano uhusisha zaidi ya mtu mmoja, ni vyema kuwa na uwezo wa kubadilika ili kuendana na hisia na matakwa ya upande wa pili wa uhusiano.

Kwa wengi, ukaribu, hasa kihisia, ni jambo linalojenga au kuharibu uhusiano.

Pia, safu hii kwa kutambua kuwepo kwa uhusiano wa kihisia na kimwili, na namna kunavyochangia kuimarisha au kuharibu uhusiano, haitasita kuzungumza hili.

Nawakaribisha sana wasomaji wangu kutoa michango yenu ya maoni kuhusiana na yale ambayo tutakuwa tunayajadili.

Pia nawakaribisha kuleta maoni ya mambo ya uhusiano ambayo hayajapata nafasi ya kujadiliwa hapa.


Ninaamini kuwa katika michango hii tutajifunza mengi.

Wiki ijayo tutaanza kuingia kwa undani suala kubwa katika uhusiano; nalo ni ndoa.

Je, umeshawahi kusikia kuhusu ndoa ambazo ndugu wa damu wanaolewa na mtu mmoja na kujenga familia zenye upendo mkubwa?

Tukutane wiki ijayo kuliangalia hilo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.



Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

Suruali za cargo zilivyobadilishwa matumizi

SURUALI za cargo au combati ni fasheni inayopendwa zaidi hasa kwa kinadada wa umri wa kati pamoja na vijana.

Suruali hizi zimeigwa kutoka kwenye m u u n d o wa kombati kwa kuwekwa mifuko zaidi ya minne, hususan pembeni ya 'hipsi.'

Suruali za aina hii hazibani sana na zilitengenezwa mahsusi kwa watu wanaofanya kazi kwenye mazingira ambayo hayapo kwenye mpangilio maalumu, ili kuwezesha kubeba vifaa vya kazi ndani ya mifuko hiyo.

Hata hivyo, fasheni hii imeibuka kupendwa zaidi na kufanywa nguo ya "mtoko maalumu" kama ilivyo suruali ya jinzi za kawaida au 'timberland.'

Asili ya suruali hizi zilizoanza kutamba tangu mwaka 1930, ni kutoka nchini Uingereza ambapo askari wake walivaa hivyo.

Kadiri miaka ilivyosonga, ndivyo vazi hili limekuwa likiboreshwa siku hadi siku na kupendwa zaidi uraiani.

Suruali ya cargo inavutia zaidi kuvaliwa na tisheti, 'kitop' kwa wadada pamoja na raba.

Namna ya kukabili ulegevu wa ngozi

UMRI unapokuwa mkubwa, ngozi yako hupunguza uwezo wake wa kawaida wa kunyumbuka na huanza kuwa ngumu.

Hii ni kutokana na kupungua kwa uwezo wa ngozi kutengeneza seli mpya na kufanya tabaka la chini ya ngozi kupungua unene wake.

Kutokana na kupungua uzalishaji wa mafuta kwenye ngozi, ngozi inasinyaa na kulegea na kukosa nuru yake ya asili.

Ufanye nini kuondoa hilo?

Tumia udongo wa mfinyanzi. Udongo huu wa asili unapatikana sehemu mbalimbali nchini ambako kuna udongo wa mfinyanzi au unaweza kuupata kwenye maduka ambayo yanauza na kutengeneza vitu asilia ikiwemo mafuta.

Matumizi

Weka udongo wako kiasi kwenye chombo kisha weka maji. Koroga kisha acha udongo ujitenge na maji.

*Nawa uso wako kwa maji safi na sabuni.

*Mimina maji hayo kwenye chombo kingine huku ukiacha udongo chini (tumia maji tu yaliyojichuja).

*Pakaa usoni na sehemu ambazo unaona ngozi imelegea ili kurudisha ubora wa ngozi mwilini wako.

*Kwa wanaofanya mazoezi, matokeo huonekana mapema zaidi. Pkaa kisha nenda kafanye mazoezi, ukirudi nawa.

*Tumia asubuhi na jioni au asubuhi tu kadri ya nafasi yako.

*Udongo wa mfinyanzi unapotumiwa ipasavyo husaidia kurejesha hali nzuri ya ngozi na kuifanya ikaze kama zamani.



Afcon



Simba, Yanga zichangamkie Pamoja Afcon 2027

Na John MARWA

IMEKUWA kawaida kwamba kila nyakati zinapokuja, hubeba sura mbili; kwamba huwasili na mambo chanya na wakati huo-huo, masuala hasi huonekana.

Wakati huu ambapo nchi tatu za Afrika Mashariki; Kenya, Uganda na Tanzania zinajiandaa kupokea mashindano makubwa ya soka kwa mataifa ya Afrika (Afcon), yatakayofanyika zaidi ya miaka miwili ijayo, 2027, inaonekana wadau wengi wa soka, hasa timu, zimelala usingizi.

Timu kubwa za Tanzania, huenda hata hazifahamu namna zinavyoweza kufaidi kuwepo kwa mashindano hayo makubwa ya kabumbu Afrika.

Mashindano hayo ambayo yanaandaliwa kwa ushirkiano wa nchi hizo na kupewa jina la Pamoja Afcon, yanakuja kuacha alama kubwa za mafanikio ambayo yatanufaisha nchi, timu, wafanyabiashara na wengine wengi ambao wataguswa moja kwa moja ama kupitia “watu wa kati.”

Serikali za mataifa yote matatu zinafanya kila jitihada kuhakikisha kunakuwepo manufaa makubwa wakati yakikaribia, yanapoanza na yanapomalizika.

Mwishoni mwa wiki iliyopiya, Julai 17, wakaguzi kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) waliwasili Dar es Salaam, Tanzania, kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Afcon, Leodegar Tenga, pamoja na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo Tanzania,

Ally Mayay.

Wakaguzi hao licha ya mazungumzo na maofisa hao, walipokea taarifa ya mpango wa serikali wa ujenzi wa viwanja vya michezo ambavyo vitatumika katika mashindano ya Afcon 2027.

Pia walitembelea baadhi ya viwanja vitakavyotumika kwenye mazoezi wakati wa michuano hiyo ambavyo ni pamoja na KMC na Meja Isamuyo, jijini Dar es Salaam.

Inavyoonekana viwanja hivyo viwili vitafaidi kuwepo kwa wachezaji wakubwa wa timu za Afrika, huku wakongwe wa soka na alama ya soka Tanzania; Simba na Yanga, zikionekana “kulala usingizi wa pono.”

Upo uwezekano mkubwa kwamba vilabu hivyo vikongwe; Simba na Yanga, vikashindwa hata kupokea senti ya maandalizi ya michuano hiyo kwa kuwa hazina kitu cha kujivunia.

Endapo timu hizo kubwa zingekuwa na viwanja bora, basi ingekuwa rahisi sana kwa shirikisho la soka Tanzania (TFF), kuishawishi CAF kuhusu kutumika kwa viwanja hivyo kwa mazoezi ya timu zitakazoshiriki.

Hata hivyo, bado kuna nafasi kwa timu hizo na hata zingine, kujipanga na kuanza mradi wa ama kuboresha viwanja vyao au kujenga upya, na kijiweka katika nafasi nzuri ya kufaidi kuwepo kwa Afcon 2027, nchini Tanzania.

Bila hivyo, timu hizo zitakuwa zikiongeza idadi tu ya watazamaji kwenye michano ya Afcon 2027, bila kufaidi pakubwa – hasa kiuchumi.



Arusha, TANZANIA

'VIBE' waliloonyesha wasanii wa kundi la muziki wa bongo fleva la Weusi, jijini Arusha limewashika mashabiki waliofika kuwatazama.

Kundi hilo linaundwa na wasanii watano akiwemo G. Nako, Joh Makini, Nikki wa Pili, Bonta pamoja na Lord Eyez.

Wakati Joh Makini akitumbui-za wimbo wake wa 'Don't Bother' aliomshirikisha marehemu AKA ilipofika 'verse' ya msanii huyo alipanda stejini Dogo Janja na kuchana mistari ya gwiji huyo kutoka Afrika jambo lililoibua shangwe kubwa kutoka kwa mashabiki waliohudhuria tamasha hilo.

Constanța, ROMANIA

MSANII wa rap kutoka nchini Marekani, Wiz Khalifa ameshindwa kabisa kuachana na tabia yake ya kutumia bangi.

Kama wahenga wanavyosema, "tabia ni kama ngozi, hivyo ni ngumu kuibadili," hilo limemkuta msanii huyo, ambaye amekuwa mara kadhaa akikamatwa na kufunguliwa kesi za matumizi ya dawa za kulevya.

Hivi karibuni msanii huyo,

alikatwa na kufunguliwa mashitaka ya kutumia na kumiliki bangi wakati akiwa stejini kwenye tamasha lililofanyika katika fukwe za bahari nchini Romania.

Wiz Khalifa alikutwa na bangi gramu 18, hata hivyo maofisa hao wa polisi walimshikilia kwa saa kadhaa na kisha kumuachia.

Baada ya kuachiwa aliomba radhi mashabiki wake kupitia ukurasa wa X, akiwaahidi kurejea tena akiwa na nidhamu.

Wiz Khalifa amekuwa 'teja'



*Aliyekuwa
kiungo wa Sim-
ba SC, Jonas
Mkude akim-
toka mchezaji
wa Sevilla
ya Hispania
kwenye mechi
ya kirafiki iliyo-
chezwa uwanja
wa Benjamini
Mkapa jijini
Dar es Salaam,
Mei 23, 2019.
(Picha na
Mtandao)*



Wadhamini Ligi Kuu wajipange

Na Mwandishi WETU

KATIKA mazingira ya sasa ya maendeleo ya mpira wa miguu, maarufu kwa jina la kabumbu au soka, mchezo huo hauwezi kusonga mbele zaidi bila wadhamini.

Udhamini wa michezo, hasa soka, una sura mbili za maana; kwanza ni manufaa kwa timu zote zinazodhaminiwa, na pia neema kwa watoa fedha wenyewe, yaani wadhamini.

Miaka nenda rudi, michano ya soka imekuwa ikidhamniwa na huenda ndiyo sababu ya mchezo huo kuwa kinara kuliko michezo mingine.

Ni kutokana na sababu hiyo, kwa upande wa Bara la Afrika, mashindano ya timu za mpira wa miguu katika Afrika Kusini imekuwa ikineemeka kwa kuwepo udhamini mnono, kuliko nchi zingine kusini mwa Jangwa la Sahara.

Ni kutokana na ukubwa wa udhamini kwa timu za Afrika Kusini, hivi karibuni wadhamini wa Kaizer Chiefs na TS Galaxy wameweza kualika timu kubwa kutoka ligi namba tatu kwa ubora barani Ulaya, Bundesliga; Augsburg na pia bingwa wa Tanzania, Yanga.

Kualika timu kubwa siyo mchezo, kunahitaji uhusiano mzuri baina ya timu, lakini kikubwa

ni fedha ili kusafirisha timu, kuitunza na mahitaji mengine wanayokubaliana.

Ni kutokana na umuhimu huo, katika Tanzania, mwaka 2017, kampuni ya SpotiPesa iliialika timu ya Everton kutoka Ligi Kuu ya Uingereza ambayo ilicheza na Simba.

Kama SpotiPesa iliweza kufanya hivyo mwaka 2017, inashindwaje leo kufanya kama hivyo? Na endapo SpotiPesa iliweza kufanya hivyo, kwa nini M-Bet, ambao wanaidhamini Klabu ya Simba washindwe kufanya hivyo leo?

Kwa nini Kampuni ya Azam, ambayo inamiliki timu ya Azam FC ishindwe kuandaa mashindano na kualika timu kutoka Ulaya kama sehemu ya maandalizi ya timu yao? Mbona Toyota wameweza kwa Kaizer Chiefs?

Kama itakuwa ni vigumu kwa mdhamini mmoja mmoja kufanya hivyo, wadhamini kadhaa wanaweza kuja pamoja na kuandaa mashindano kama hayo ili kupunguza mzigo wa gharama.

Pamoja na kuwatengenezea wadhamini fedha, lakini mashindano hayo yatazipa timu kipimo sahihi wakati zikiajiandaa kwa mashindano ya kimataifa.

Ni vyema sasa na kwa hakika upo umuhimu wa wadhamini wa timu za Tanzania, kuangalia uwezekano wa kuandaa michezo ya kujipima nguvu kama haya yaliyoandaliwa na timu za Afrika Kusini ili kuwapa uzoefu wachezaji na wakati huohuo, wadhamini wakifaidi kufahamika.

MICHEZO

Jumatatu, Julai 22-28, 2024



Tanzania ijifunze Afrika Kusini kuandaa timu



Kiungo wa Yanga SC, Stephane Azizi Ki akijaribu kumtoka mchezaji wa FC Augsburg kwenye mechi iliyochezwa nchini Afrika Kusini juzi. Yanga ilifungwa 2-1 (Picha na Mtandao)

Na Mwandishi WETU

TIMU za madaraja yote nchini Tanzania kwa sasa zipo kwenye maandalizi ya msimu ujao wa ligi.

Katika ligi kuu, ukiondoa Simba na Azam ambazo zimesafiri nje ya nchi kwa ajili ya maandalizi hayo, timu nyingine zote zimeweka kambi zao hapa nchini.

Maandalizi yanayofanywa yanahusisha masuala ya mbinu yakilenga kuwawezesha makocha kujenga vikosi imara.

Timu nyingi zimefanya usajili wa wachezaji kadhaa na nyingine ziliajiri makocha wapya.

Hivyo kipindi hiki kinatumika na walimu wa mpira kuweka misingi na mbinu watakazotumia ligi zitakapoanza.

Kwa kawaida, mandalizi ya timu nyingi hupenda kucheza mechi za majaribio kama kipimo kwa kocha na wachezaji.

Mechi hizi ni muhimu kwani zinampa kocha kipimo cha kuona mafunzo yake 'yameingiaje' kwa wachezaji, hasa wapya.

Ingawa inasemwa kuwa matokeo siyo jambo linaloangaliwa sana kwa walimu katika kipindi hiki, hivyo kuamua kucheza na timu hata za madaraka ya chini, lakini upo umuhimu wa kuwapitisha wachezaji walio katika mandalizi kwenye 'tanuru la moto' kwa kuwapatia mechi na timu nyingine mahiri.

Timu mbili za Afrika Kusini, TS Galaxy na Kaizer Chiefs zimeandaa mashindano ya kimataifa na kuzialika timu kadhaa, zikiwamo Yanga na Augsburg, inayoshiriki ligi kuu kuu nchini Ujerumani.

Hivyo limekuwa ni jambo la faraja kuwa Yanga, ambayo ilianza kambi yake ya maandalizi Avic Town jijini Dar es Salaam, imepata mwaliko kwenda Afrika Kusini kushiriki mashindano mawili tofauti ya maandalizi ya msimu mpya.

Katika mashindano hayo Yanga imeshakutana na timu ya Augsburg, na pia ilicheza na Kaizer Chiefs.

Hizi ni miongoni mwa timu kubwa barani Ulaya na Afrika, hivyo ni sahihi kusema kuwa ni kipimo kizuri kwa Yanga ambayo pamoja na ligi inajiandaa pia kwa mashindano ya Klabu Bingwa Barani Afrika.

Simba kwa upande wake yenyewe iko Misri wakati Azam iko Morocco. Huko wanafanya maandalizi yatakayohusisha mechi kadhaa za kirafiki, lakini na timu za madaraja ya chini.

Kwa msingi huo tunapata somo zuri sana kutoka Afrika Kusini ambako timu za TS Galaxy na Kaizer Chiefs zimeandaa mashindano yanayotumika kama maandalizi ya msimu ujao.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

